Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



Uk. 24

## Stars kuandika wasifu mpya?

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00048 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Januari 24 - 30, 2024 |

## Rais aipa gari Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa



**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ameendelea na jitihada za kuimarisha taasisi muhimu nchini baada ya kuipa Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, gari la kisasa ili itumike kuboresha utendaji kazi katika sekta ya afya. *Uk. 3*

## Mtoto atolewa skurubu kwenye mapafu



Uk. 3

## Tanzania yapongezwa utekelezaji mradi wa JNHPP

Uk. 2



## Serikali hii inayofanya makubwa haichafuliki kitoto

Uk. 12



# ‘Samia ni vitendo zaidi, si maneno’

- Hutoa majawabu ya changamoto za wananchi



Uk. 4

## ... Amefanya mengi kwa muda mfupi

Uk. 4

# TADB: Rais Dk. Samia amedhamiria vijana waendeshe kilimo biashara

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

MKURUGENZI Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, amesema lengo la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni kuiimarisha benki hiyo ili iwasadie vijana kuendesha kilimo biashara, kuongeza ajira na kuwa na usalama wa chakula.

Nyabundege aliyasema hayo kabla ya zoezi la kugawa vifaa na zana za kilimo kwa vijana 268 walio katika program ya Building a Better Tommorow (BBT) katika shamba la pamoja la Chinangali 11 jijini Dodoma juzi.

Alisema wakati Rais Dk. Samia anaingia madarakani, benki hiyo ilikuwa na mtaji wa Sh. bilioni 60, hivyo ilikuwa ikishindwa kufikia watu wengi kwa sababu ya uwezo wa kifedha.

"Mwaka ule wa kwanza alipofika 2021, aliiongezea fedha benki hiyo mtaji wa Sh. bilioni 208 na mwaka 2022, Rais katika diplomasia yake ya uchumi anapokwenda kutafuta fedha katika Jumuiya za Kimataifa, hakuisahau, aliipatia Sh. bilioni 210 kutoka Shirika la Fedha la Ufaransa," alisema Nyabundege.

Aliongeza kuwa pia katika mwaka wa fedha 2023/2024, TADB imepatiwa mtaji wa Sh. bilioni 170 na kwamba Rais Dk. Samia anaimarisha benki hiyo ili kusaidia vijana.

Aliwataka vijana kujitambua ili kuhakikisha wanapata maisha bora kwani program hiyo imekusanya vijana kutoka maeneo mbalimbali

"TADB ni benki yenu, njooni tutawasaidia, fedha za kuwawezesha zipo TADB inatoa mtaji kwa riba ndogo, tumepata Rais aliyeamua kutoa fedha na raslimali kuhakikisha vijana wanapata ajira na mitaji," alisema.

Jumla ya vijana 268 waliopo kwenye program ya BBT, walikabidhiwa zana za kilimo na barua za umiliki wa mashamba tayari kwa ajili ya kuanza uzalishaji.

Akizungumza na vijana hao, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, alisema maono ya Rais Dk. Samia yametimia.

Alisema Rais amekuwa akihakikisha vijana wanajiinua kiuchumi kwa kukuza ajira na kuongeza tija kwenye kilimo.

"Vijana walikuwa hawana ardhi, mitaji na ujuzi, rai ya Rais ni kuona vijana wanashiriki kwenye kilimo na kuwa na usalama wa chakula, kujilisha wenyewe na kuwalisha wengine kibiashara," alisema Profesa Ndalichako na kuongeza:

"Hii ni program ambayo ndani yake kuna miradi mingi ya kilimo na ufungaji. kunenepesha mifugo na wametoa elimu kwa vijana zaidi ya 500 na Ofisi ya Waziri Mkuu, imetia Sh. milioni 981 kwa ajili ya kuwezesha vijana."

Kwa upande wake, Waziri wa Kilimo Hussen Bashe, alisema wakati programu hiyo ikianza, watu walikuwa na maneno mengi ya kukatisha tamaa.

"BBT siyo mradi, ni programu yenye malengo matatu ikiwemo kutengeneza ajira, kupunguza umaskini na kuongeza tija," alisema na kuongeza:

"Baada ya kuwa viongozi kuwalaumu vijana kila siku, tulifanya tathmini tukagundua vijana hawalimi kwa vile hawana ardhi, lazima awe na teknolojia itakayomfanya alime, lazima awe na mfumo rafiki wa fedha unaoweza kumpatia mtaji."

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri, alisema Rais Dk. Samia aliamua kilimo kiwe na mabadiliko .

"BBT ni programu yenye mambo matatu ndani yake ambayo ni kuwachukua vijana waliopo mtaani na kisha kuwafundisha kilimo na kuwapatia mashamba, pia inashirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambapo vijana 200 wanapewa kozi fupi na kwenda kusimamia shughuli za kilimo na wakulima ambapo hawa ni wakulima wanaolima kila siku, lakini wanakabiliwa na changamoto za masoko, ukosefu wa vifaa na elimu ya kilimo," alisema

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Biashara, Mifugo na Uvuvi, Deo Mwanyika, alisema: "Hizi ni fedha za umma zinatoka Serikali Kuu na zinakopwa.

Alisema Kamati ya Bunge ni kuishawishi serikali kutoa fedha na Rais aliongeza bajeti kwenye Wizara ya Kilimo.



Katibu Mkuu CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, akikabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, Daniel Chongolo (kulia) jijini Dodoma jana.

## Misri yaipongeza Tz utekelezaji mradi wa JNHPP

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nyumba, Nishati na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Assim Elgazzar, ameipongeza Tanzania kwa kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) ambao umefikia asilimia 95.83 hadi sasa.

Waziri huyo alitoa pongezi hizo juzi baada ya kutembelea mradi huo uliopo Rufiji mkoani Pwani akiwa amefuatana na mwenyeji wake, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga.

Alisema Serikali imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa mradi huo wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere ambao utasaidia kuondoa changamoto za upatikanaji wa umeme nchini.

"Maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu ni mazuri na ndani ya muda mfupi ujao, tunatarajia kuona mradi huu ukikamilika na kumaliza kabisa changamoto ya umeme hapa nchini," alisema Elgazzar.

Alisema Serikali ya Misri inataka kuona mradi huo ukikamilika kwa wakati na ufanisi mkubwa ambapo Misri itaendelea kutoa ushirikiano kwa makandarasi katika hatua zote za utekelezaji wa mradi huo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati Judith Kapinga, alisema kuwa Waziri Elgazzar ametumwa na Rais wa Misri kuja kuangalia maendeleo ya mradi huo unaojengwa na Kampuni ya JV Elsewedy na Arab Contractor kutoka Misri.

Wengine walioshiriki katika ziara hiyo ni Mkurungenzi Mkuu wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati.



## RC : Temesa tembeleeni taasisi zilipe madeni

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Elias Thomas, ameutaka uongozi wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (Temesa) mkoani hapa, kuacha kujifungia ndani bali watembelee na kushirikiana kwa karibu na taasisi zote ili zilipe madeni yao.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wadau wanaotumia huduma za Temesa mkoani hapa.

Kikao hicho kilichohudhuriwa pia na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Wakurugenzi wa Wilaya pamoja na wakuu wa taasisi zilizoko mkoani hapa, wauzaji wa vipuri, wamiliki wa gereji binafsi pamoja na washitiri kutoka mashirika mbalimbali.

"Temesa mnahudumia taasisi za Serikali, tokeni, mpite muende kwenye zile taasisi mnazozihudumia, zungumzeni nao, mjue ziko wapi, mjue wana changamoto gani, mshauriane nao ili muone ni jinsi gani wanaweza kulipa madeni mnayowadai, lakini muweka nao mpango mkakati mzuri wa kutengeneza magari yao," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Elias Thomas.

# Mtoto atolewa skurubu kwenye mapafu

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa mara nyingine, imefanikiwa kutoa skurubu kwenye mapafu ya mtoto.

Hii ni mara ya tatu kwa MNH kufanikiwa kuwaondoa wagonjwa vitu vilivyowakwama katika mapafu yao kwa kutumia kifaa maalum.

Katikati ya mwezi huu, mtoto mwenye umri wa miaka mitano, aliondolewa shanga ya plastiki katika pafu lake la kulia na juzi hospitali hiyo ilifanikiwa kuondoa ganda la pipi kwenye pafu la kushoto la mama mwenye umri wa miaka 53 lililodumu nalo kwa miaka 11.

Katika tukio la juzi kwa mujibu wa mtandao wa Instagram wa hospitali hiyo, mtoto huyo alikuwa akichezea skurubu kinywani kwake wakati akiwa shule na kwa bahati mbaya ikaimeza na ikamkwama kwenye mapafu.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mapafu na Mfumo wa Upumuaji kutoka MNH, Mwanaada Kilima, alisema mtoto huyo alipaliwa na skurubu hiyo siku nne zilizopita ambayo iliingia kwenye mapafu yake.



# Samia aipa gari Hospitali Wilaya



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ruangwa (mwenye suti kushoto), Fabian Chonya, akishangilia na watumishi wa Idara ya Afya ya wilaya hiyo baada ya kukabidhi gari lililotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Picha ya chini akimkabidhi gari mmoja wa maofisa wa Idara ya Afya wa wilayani humo.

Inatoka uk. 1

Akizungumza wakati wa kukabidhi gari kwa maofisa wa hospitali hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Frank Chonya, alisema Rais Dk. Samia anaendelea kupigania maisha ya watu kwa vitendo.

"Rais Dk. Samia ameagiza gari hii itumike kuharakisha watoa huduma kuwafikia wagonjwa popote walipo ili kusaidia kuokoa maisha yao," alisema Chonya mbele ya watumishi wa kada ya afya wilayani hapa.

Alisema Ruangwa imepokea gari hilo aina ya Toyota Land Cruser lenye namba za usajili STM 794, wakati hospitali ikiwa na madaktari bingwa wakisubiri wananchi wawahudumie kibingwa.

Mkurugenzi Chonya alimshukuru Rais Dk. Samia akisema amekuwa akiikumbuka Wilaya ya Ruangwa kila wakati, huku akiwaasa wakazi wa wilaya hiyo kuendelea kumuunga mkono aifikishe wilaya katika mafanikio ya juu kimaendeleo.



# Amani, utulivu kuchagiza maendeleo Z'bar

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

MWAKILISHI wa Jimbo la Makunduchi, Haroun Ali Suleiman, amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuendeleza ushirikiano katika kudumisha amani na utulivu uliopo nchini ili kuchagiza maendeleo ya haraka.

Alitoa rai hiyo Makunduchi Wilaya ya Kusini juzi wakati akifunga mafunzo ya vijana ya itikadi katika tawi la Muyuni A, Kajengwa B na Miwaleni Mkoa wa Kusini Unguja. Alisema ushirikiano wa pamoja utakiwezesha CCM kuendelea kupata ushindi katika uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge, wawakilishi na madiwani, unaotarajiwa kufanyika 2025.

Aidha, aliwataka vijana hao kuwa wazalendo na kuhakikisha wanayafanyia kazi mafunzo waliyopatiwa ili kuleta tija kwao, pamoja na kuiletea maslahi CCM na Taifa kwa jumla. Pia aliwataka kuendelea kukinadi na kuhamasisha sera za CCM kwani Ilani ya Chama inatilia mkazo maendeleo ya vijana katika nyanja mbalimbali ikiwamo kuwawezesha kuzifikia fursa ajira zitokanazo na Uchumi wa Buluu.

# Zaidi ya nusu ya watoto Njombe wana udumavu

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

ASILIMIA 50.4 kati ya watoto 114.000 mkoani Njombe, wametajwa kuwa na udumavu, hali inayosababisha washindwe kufanya vizuri katika masomo yao shuleni.

Aidha, asilimia 12 kati ya watoto hao, wanakabiliwa na changamoto ya uzito pungufu na zaidi ya asilimia mbili wanaelezwa kuwa na hali ya ukondefu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Juma Mfanga, aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha lishe na mpango wa kuongeza kasi ya kupunguza udumavu mkoani humu uliofanyika katikiakatika mkoa hapa ambao uliofanyika katika Mji Mdogo wa Makambako.

Alisema changamoto ya udumavu inasababishwa na wazazi kushindwa kuwaandalia watoto wao chakula bora na kuwaachia makande na viazi huku muda mwingi wakiutumia kwenye shughuli za kiuchumi na wengine starehe.

Kwa upande wake, Afisa Lishe wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makambako, Meckfrida Mmari, alisema changamoto kubwa ambayo inasababisha udumavu kwa watoto, ni wanaume kutelekeza familia na kusababisha wanawake wahangaike na malezi ya watoto wao na kutafuta uchumi peke yao kutokana na kubeba mzigo mkubwa wa kulea familia.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makambako ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Kitandililo, Imani Fute, alisema iko haja ya kutungwa kwa sheria ya kuwabana wanaume kuhudhuria kliniki ili wapate elimu juu ya malezi ya watoto wao wakiwa tumboni.

Naye Diwani wa Kata ya Majengo, Rosemary Lwiva, alisema udumavu ni chanzo cha wanafunzi kukimbia masomo ya sayansi.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi mjini Makambako waliokuwa kwenye tukio hilo, walisema changamoto kubwa kwao ni namna ya kuandaa chakula bora.

# 'Samia ni vitendo zaidi, si maneno'

## ■ Hutoa majawabu ya changamoto za wananchi

**Na Sifa Lubasi, Dodoma**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni wa vitendo zaidi na siyo maneno na kwamba unatoa majawabu ya changamoto zinazowakabili Watanzania.

"Rais Dk. Samia amekuwa haangalii tatizo, lakini amekuwa akiangalia zaidi utatuzi wa tatizo," alisema.

Aliyasema hayo jijini Dodoma jana wakati wa uzinduzi wa Taasisi ya Usuluhishi na Malalamiko ya Taarifa za Kodi (TOSTI).

"Watanzania waweke kumbukumbu kwa vitu vilivyokuwa vinapigiwa kelele na vikachukuliwa hatua. Rais Samia anafanya mambo mengi ambayo yanatakiwa kwenye kumbukumbu. Mtakumbuka kulikuwa na malalamiko kuhusu haki za watu, nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Rais akasema si vizuri wakazungumza tu na ndipo aliamua kutengeneza timu ambayo iliibua vitu vingi," alisema.

Alisema Rais Dk. Samia anataka kuona jambo fulani linatekelezwa huku mwenyewe akitafuta ufumbuzi wa matatizo hayo.

Kuhusu TOSTI, Waziri Dk. Nchemba alisema kuanzishwa kwa taasisi hiyo kutasaidia kukuza uchumi na mapato.

Alisema huwezi kuzungumzia maendeleo bila kulipa kodi.

"Deni la serikali halilipwi kwa kuuza ng'ombe kwenye ranchi, watu lazima walipe kodi, janja janja ya kukwepa kodi kunaahirisha tu tatizo," alisema.

Alisema yeyote anayetakiwa kulipa kodi halali, lazima alipe kodi halali na anayetakiwa kutoza kodi atoze kodi halali.

"Rais Samia aliona kuwa anayekadiria kodi na anayekatiwa rufaa, ni yule yule, anayekadiria inamshawishi kujenga mazingira ya rushwa kwa vile hakuna mbadala, tunaamini hilo litafanyiwa kazi," alisema.

Aliitaka taasisi hiyo na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukaa pamoja na kubainisha sheria na kanuni zinazowakwamisha kwani watakuwa hawamtendei haki Rais Dk. Samia kama ofisi inaanzishwa, lakini malalamiko yakawa pale pale.

Alisema katika jukumu la kukuza uchumi TRA wafanye kazi kwa weledi, lakini ofisi hiyo itasaidia kupunguza malalamiko.

"TRA mzingatie weledi, sheria na mtu alipe kodi anayostahili asibambikiziwe kodi, lakini taasisi inatakiwa kusaidia katika hilo," alisema.

Alisema katika suala la kukusanya mapato, nchi zilizoendelea walishavuka huko, hawana utani wala mzaha katika masuala ya kodi na nidhamu ya kiongozi kwa mwananchi wa kawaida iko kwenye masuala ya kodi hakuna mkubwa, mdogo wala mtu maarufu.

"Wenzetu walioendelea na sisi tunatamani tuwe kama wao moja ya eneo ambalo hawana mjadala nao ni kodi, lazima tukusanye kodi na lazima tujenge uchumi , haya ni maeneo yenye umuhimu unaolingana, sisi bado tunapata shida sana katika maeneo hayo, tunatarajia taasisi hii itusaidie kwenye jambo hili," alisema.

"Ukienda kwenye takwimu zote za walipa kodi hazituweki pazuri sana ukiangalia uwiano na pato letu havifanani.

Tuna kazi ya kufanya katika masuala ya kulipa kodi kwa sababu tumeamua na ipo kwenye kaulimbiu na miongozo yetu lazima tujenge taifa linalojitegemea," alisema na kuongeza:

"Siyo heshima kwa nchi kama Tanzania, kutegemea misaada, barabara zote ni fedha zetu, tunatamani kuwa na barabara za lami hadi ngazi za vijiji, kuwe na shule bora hadi vijijini."

Alisema sasa hivi kuna shule za viwango vijijini, zina marumaru na madirisha ya vioo, kwenye huduma za maji walianza na kumtua mama ndoo kichwani sasa maji yapatikane walipo wananchi lazima kodi ikusanywe.

Kwa upande wake, Msuluhishi wa Mamlaka ya Kodi, Robert Manyama, alisema marekebisho ya sheria yalitoa mamlaka ya kupokea maboresho ya mfumo wa ukusanyaji kodi na kuongeza ukusanyaji kodi wa hiari.

Manyama alisema Ofisi ya Msuluhishi wa Malalamiko ya Kodi kwa sasa iko Dodoma pekee na jitihada zinaendelea ili kusogeza huduma jijini Dar es Salaam.

Alisema juhudi zinazendelea kupata wafanyakazi watakaosimamia malalamiko kwa weledi.

Alitaja utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kwa msuluhishi kwa mmoja anaweza kutumia namba 0800111022, 0808110100 au kwa barua pepe.

Aidha, njia nyingine za kuwasilisha malalamiko ni kwa kutumia njia ya posta na kufika kwenye ofisi ya taasisi hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, alisema Juni 19, mwaka jana, Bunge lilipitisha Sheria ya Fedha ili kuanzisha ofisi hiyo, sheria hiyo ilianza kutumia Julai 19, 2019, lakini haikufaya kazi mpaka leo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema Rais Dk. Samia ana dhamira ya dhati ya kukusanya fedha na kuzigawa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema yote yanatokea kwa kuwa Rais Dk. Samia amekuwa na utashi wa kipekee, walipa kodi, wafanyabiashara wanalipa kodi kwa utashi.

"Miradi inayokuja Dodoma ni ya kihistoria ambayo haijawahi kushuhudiwa," alisema.

Alisema ujio wa taasisi hiyo utaleta haki na malalamiko ya kodi yatatatuliwa kwa wakati.



**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.**

# ...Amefanya mengi kwa muda mfupi

**Na Mwandishi Wetu, Simanjiro**

MBUNGE wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka, amesema katika maisha yake, ameshuhudia Marais watano wakiongoza Tanzania, lakini hajawahi kuona Rais aliyefanikisha maendeleo kwa muda mfupi kama Dk. Samia Suluhu Hassan.

Akitoa ushuhuda, Sendeka alisema alishika nyadhifa mbalimbali nchini tangu Awamu ya Kwanza, enzi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, lakini hajawahi kushuhudia miradi mingi ya maendeleo kama inavyofanywa hivi sasa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye Wiki ya Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania, huku benki ya CRDB ikipanda miti 500 kwenye zahanati ya Nakweni wilayani Simanjiro kwa lengo la kutunza mazingira na kurejesha uoto wa asili.

Alisema Rais Dk. Samia amefanikisha miradi mingi ya maendeleo kwenye sekta ya elimu, afya, maji, umeme na miundombinu ya barabara nchini kwa muda mfupi aliyoongoza nchi kuliko Rais yeyote, hivyo mwaka 2025, Watanzania wanapaswa kumuongezea kipindi kingine cha miaka mitano zaidi.

"Nilikuwa Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Kiteto Awamu ya Kwanza ya Nyerere, nilikuwa Ofisa Tarafa Awamu ya Pili ya Ali Hassan Mwinyi, nilikuwa Mkuu wa Utawala UVCCM Taifa Awamu ya Tatu ya Benjamin William Mkapa, Mbunge Awamu ya Nne ya Jakaya Mrisho Kikwete, Msemaji wa CCM na Mkuu wa Mkoa wa Njombe na Awamu ya Tano ya John Joseph Magufuli. Sijaona Rais aliyeleta maendeleo kama Dk. Samia," alisisitiza Sendeka.

Aidha, alifafanua kwamba wanachama wa CCM na viongozi wa vyama vya upinzani, wanapaswa kujiandaa kisaikolojia wakitambua kuwa Rais Dk. Samia ataendelea kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

"Nitazunguka katika wilaya na mikoa ya jamii ya wafugaji na kuimba mema yote na mazuri yaliyofanywa na Rais Dk. Samia tangu ashike madaraka ya kuongoza nchi," alisema.

Hata hivyo, katika tukio hilo, Ole Sendeka alituzwa fedha na kalamu ya wino na viongozi wa dini wakiwamo Maaskofu na Masheikh baada ya kughani wimbo wa kumpongeza Rais Dk. Samia.

> **"Nilikuwa Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Kiteto Awamu ya Kwanza ya Nyerere, nilikuwa Ofisa Tarafa Awamu ya Pili ya Ali Hassan Mwinyi, nilikuwa Mkuu wa Utawala UVCCM Taifa.**

# `Shirikianeni na vyombo vya ulinzi na usalama'

**Na Mwandishi Wetu, Singida**

MBUNGE wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, amewaomba wafanyabiashara wa Mji wa Ikungi kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama baada ya kituo kipya cha magari kuhamishiwa Kijiji cha Muungano.

Amesema anafahamu bado kuna kero za mazingira ya biasahara wakati miundombinu ya kituo hicho ikiwa bado hakijakamilika ikiwamo muda wa kufunga biashara za vinywaji.



Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu.

"Lengo la mkutano huu, ni kuwasisitiza muendelee kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na kusikiliza kero zenu wafanyabiashara na kuzitafutia ufumbuzi kupitia mamlaka ya Serikali," alisema.

Alisema ushirikiano huo utasaidia kulinda amani ili kuvutia wateja kuja kwenye mji wa Ikungi na hivyo kuwaongezea mzunguko wa biashara zao na kukuza uchumi wa wananchi.

Mtaturu alisema mbali na kushirikiana na vyombo vya ulinzi wanatakiwa kuimarisha uongozi wao ili kurahisisha kuwasilisha changamoto zao kwa pamoja kwenye mamlaka zinazosimamia biashara katika mji huo.

Aidha, aliwahakikishia kuwa changamoto zao ikiwemo ya kurekebisha maegesho ya magari makubwa kando ya barabara, kuweka vivuko sehemu palipojengwa barabara za lami kwenye mitaa, kuweka milango kwenye vyoo vya kituo kipya na kuruhusu malori kuegesha maeneo yaliyokuwa kituo cha magari cha zamani zitatatuliwa.

Afisa Mazingira, Richard Rwehumbiza, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri, alimshukuru Mbunge kwa kuitisha mkutano huo uliowakutanisha na wafanyabiashara wa Mji wa Ikungi na kupokea changamoto zilizoainishwa na wafanyabiashara na kuzifanyia kazi ikiwemo kuweka milango kwenye vyoo vya kituo kipya kwa kuwa fedha zipo.

"Kuhusu stendi ya zamani kurekebishwa kwa kuwekwa kifusi ili malori yaweze kuegeshwa nalo lipo kwenye mpango wa halmashauri, tunakuomba Mbunge wetu utupe ushirikiano," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara kuendelea kuzingatia masharti ya leseni zao na kushirikiana kuweka mji safi kwani kuna mpango wa kununua trekta kwa ajili ya kubeba taka ngumu.

> Lengo ni kuunganisha kipande cha lami cha kilomita saba kilichojengwa awali.

# Bashungwa aitwisha zigo Tanroads Njombe

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amemuagiza Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Njombe, kuendeleza ujenzi wa kilomita mbili za barabara ya lami kila mwaka kutoka Kijiji cha Ujuni hadi Mjini Makete.

Alitoa agizo hilo juzi katika Kata ya Kitulo Kijiji cha Ujuni alipotembelea na kukagua ujenzi wa barabara ya kutoka Makete hadi Isyonje kwenda mkoani Mbeya umbali wa kilomita 36.3.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa.

Alisema lengo ni kuunganisha kipande cha lami cha kilomita saba kilichojengwa awali.

Aidha, alimuagiza Kaimu Mkurugenzi wa Miradi wa Tanroads, Jephason Nnko, kuwachukulia hatua wakandarasi wote nchini wanaokiuka mikataba ya ujenzi huku kampuni ya Avic International inayojenga barabara ya Makete-Isyonje Mbeya kutakiwa kupeleka mitambo yote ndani ya wiki tatu.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema Kata ya Kitulo inazalisha viazi vinavyosaidia kupaisha makusanyo ya ndani ya halmashauri ya Sh. milioni 700, hivyo ni muhimu kujengwa kwa barabara hiyo.

Awali, Diwani wa Kata ya Kitulo, Abely Mahenge, aliwasilisha maombi kwa Waziri ya kujengwa kwa barabara hiyo ambayo ni muhimu katika kukuza uchumi ikiwamo usafirishaji wa viazi mbatata vinavyolimwa kwa wingi katika eneo hilo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Makete, Festo Sanga, alisema matumaini yake ni kwamba serikali itaendelea kujenga barabara hizo kama ambavyo ujenzi unaendelea mahali tofauti nchini.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Polisi toeni huduma bora



Mpaka leo polisi wameshindwa kumwona raia anayefika vituoni mwao kwa kutaka huduma mbalimbali kama mteja bali mtu wa kusukumwa sukumwa tu.

Hii ni kutokana na majibu na wala kutoandaa mabenchi kwa ajili ya wananchi kukaa wakati wakisubiri huduma mbalimbali.

Juzi pale kituo cha Chang'ombe nilishuhudia askari waliokuwa kaunta wakihoji na kutoa majibu yasiyoridhisha kwa wananchi wengi waliofika kutaka huduma kuonesha kwamba hawana kile wazungu wanaita customer care.




## MAONI YA MHARIRI

# Hongereni Muhimbili

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MHN), ndiyo hospitali kubwa hapa nchini na tegemeo kwa Taifa. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imefanya maboresho makubwa katika hospitali za rufaa, kanda, mikoa, wilaya, vituo vya afya na zahanati kuanzia majengo, vifaa tiba na dawa.

Kwa hakika, kwa mwenye macho, haambiwi tazama kwani kila kilichofanywa na Rais Dk. Samia katika sekta ya afya, kinaonekana.

Kutokana na maboresho hayo, sekta ya afya kwa ujumla wake, imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, lakini kipekee, UELEKEO inachukua nafasi hii kuipongeza Hospitali ya Taifa Muhimbili chini ya uongozi wa Mkurugenzi wake Mkuu, Profesa Mohamed Janabi.

Katika kipindi cha takribani wiki moja, madaktari bingwa wa MNH, wamefanya mambo kadhaa ya kuokoa uhai wa Watanzania wenzetu.

Tukio la kwanza la hivi karibuni, ni pale Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Mapafu na Mfumo wa Upumuaji, walipofanikiwa kuondoa shanga ya plastiki katika pafu la kulia la mtoto mwenye umri wa miaka mitano.

Ilielezwa kuwa mtoto huyo alipatwa na masahibu hayo alipokuwa akichezea shanga hiyo na kwa bahati mbaya iliimeza na ikaendea moja kwa moja kwenye pafu na kuanza kumsumbua.

Wakati watu wakitafakari hilo, MNH ikatoa taarifa nyingine kwamba mabingwa wake wamefanikiwa kuondoa ganda la pipi kwenye pafu la kushoto la mama mwenye umri wa miaka 53 alililodumu nalo kwa miaka 11.

Kana kwamba hiyo haitoshi, juzi tena MNH ikautangazia umma wa Watanzania kuwa mabingwa hao wamefanikiwa tena kuondoa skurubu kwenye mapafu ya mtoto.

Mtoto huyo ilielezwa kwamba wakati akiwa shuleni, alikuwa akichezea skurubu hiyo kinywani mwake na kwa bahati mbaya ilitelezа kisha ikaingia tumboni mwake na kumkwama kwenye mapafu.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mapafu na Mfumo wa Upumuaji kutoka MNH, Mwanaada Kilima, alisema baada ya mtoto huyo kupaliwa na skurubu hiyo, alifikishwa hospitalini hapo na ndipo madaktari bingwa walipofanikiwa kuiondoa na kuokoa maisha yake.

UELEKEO tunasema haya ni mafanikio makubwa kwa watalaamu wetu wa MNH na tunapenda kuwapongeza kwa niaba ya Watanzania.

Inatia moyo kuona kwamba baada ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Rais Dk. Samia, sasa Watanzania wanaanza kufaidi matunda yake.

Tunawaomba madaktari bingwa mwendelee na jitihada hizo kwani mbali ya kuokoa maisha ya Watanzania wenzenu, pia mnaokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kingetumika kuwasafirisha nje ya nchi wakapatiwe tiba na sasa fedha hizo zinatumika kwa shughuli nyingine za maendeleo.

Lakini tunawaomba wazazi pia kuwa makini na watoto wadogo kuhakikisha hawaweki vitu mdomoni au puani zikiwemo pesa za sarafu kwani kuna matukio kadhaa yakiwemo yalitatuliwa na MNH ya watoto kujikuta vitu hivyo vikiteleza na kuingia tumboni na kuwaleata matatizo.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com

## JICHO LANGU

Na Abdul Mitumba, Ruangwa

# Bado hali si shwari usawa wa kijinsia

LICHA ya Tanzania kufanikiwa kuwa na Rais mwanamke wa kwanza kushika wadhaifa huo wa juu tangu tupate uhuru mwaka 1961, bado mengi yanapaswa kufanyika ili kuwa na wanawake wengi zaidi katika ngazi za maamuzi.

Mara kadhaa, nimeshuhudiwa chaguzi zisizo huru na haki kama utazitazama kwa jicho la kijinsia. Pia bado mienendo, sheria, sera na mipango isiyozingatia jinsia imeacha iendelee kufanya kazi.

Baadhi ya sheria zinazolalamikiwa, mintarafu suala la jinsia kwenye chaguzi ni pamoja na sheria ya uchaguzi, sheria ya ndoa inayohalalisha ndoa za utotoni na sheria ya vyama vya siasa isiyowajibisha vyama kuzingatia usawa wa kijinsia katika uongozi wa vyama na uteuzi wa wagombea.

Kutokana na changamoto hizo, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), umelazimika kueleza wazi madhara yatokanayo na kuendelea kuwepo kwa vitendo na matukio yanayobeba mfumo dume dhidi ya wanawake hasa tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

TGNP inasema ukatili dhidi ya wanawake na wasichana bado ni tatizo kubwa hapa Tanzania, hasa ikizingatiwa ukatili huo hutumika kama njia ya kudhibiti na kukandamiza wanawake.

Pamoja na kuwepo na jitihada mbalimbali za kutokomeza ukatili na kukosekana kwa usawa wa kijinsia, bado takwimu zinaonesha kuendelea kuwepo kwa tatizo hilo.

Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukali Dhidi ya Wanawake na watoto Tanzania wa mwaka (2017/2018-2021/2022), ulibaini kwamba wanawake katika ngazi zote hupitia aina nyingi za ukatili ikiwa ni pamoja na kuumizwa kimwili, kisaikolojia, kingono ikiambatana na rushwa ya ngono.

Na takwimu za hivi karibuni kabisa zinaonesha kwamba; asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 wameumizwa kimwili, ambapo asilimia 17 kati yao wameumizwa kingono.

Kati ya wanawake wenye umri huo, asilimia 44 wamepitia ukatili wa kingono au kimwili, mara nyingi zaidi kutoka kwa wenzi wao.

> **Vilevile, taarifa mbalimbali za wachunguzi wa chaguzi zilizopita zilionesha kuwepo kwa ukatili dhidi ya wanawake hususani wagombea wa nafasi mbalimbali.**

TGNP kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya Wanawake inasema ukatili unaofanywa na watu wenye mahusiano ya karibu ni mkubwa zaidi hasa vijijini ambapo asilimia 52 wameshapitia kwenye ukatili ukilingatisha na mijini ambako ni asilimia 45 tu.

Takwimu zinaonyesha kuwa karibu asilimia 30 ya wasichana walio chini ya miaka 18 wamenyanyasika na kuumizwa kingono.

Takwimu zilizokusanywa na Chama cha Waanidishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), zilibainisha kwamba takribani asilimia 89 ya wanawake katika sekta binafsi wanadaiwa rushwa ya ngono kama sharti la kupata ajira au kupandishwa vyeo.

"Vilevile, taarifa mbalimbali za wachunguzi wa chaguzi zilizopita zilionesha kuwepo kwa ukatili dhidi ya wanawake hususani wagombea wa nafasi mbalimbali," imesema sehemu ya Ilani hiyo.

TGNP na washirika wake wamebainisha madai yao hususani ya ushiriki kwenye chaguzi mbili zijazo, yaani wa mwaka huu wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji na ule Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Wanaitaka serikali itumie idara za taasisi zake katika kuweka sawa uwanja wa ushindani na hususani kuweka taratibu za kuwezesha kufikia lengo la 50/50 kwenye uongozi.

# ZIARA YA KATIBU WA ITIKADI, UENEZI NA MAFUNZO WA CCM MKOANI TANGA















# Samia kafikisha tabasamu jijini Mbeya - Dk. Tulia

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

NI Januari 22, 2024 siku ambayo wanafunzi 3,000 wa shule za msingi za Jiji la Mbeya kutoka kwenye familia zenye changamoto za kiuchumi, wanatabasamu.

Wanatabasamu baada ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson (CCM), kufanya hafla maalum ya kutangaza kuwakabidhi sare za shule na madaftari ya masomo yote kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la nne.

Dk. Tulia ambaye pia ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), anasema tabasamu hiyo inaonekana kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awainayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.



**Mbunge wa Mbeya Mjini ambaye pia ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, akizungumza kwenye hafla ya kuwakabidhi vifaa vya shule wanafunzi 3,000 jijini Mbeya.**



**Baadhi ya wanafunzi waliofika kupokea vifaa vya shule vilivyotolewa na Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson.**

Anasema Rais Samia ameleta tabasamu Mbeya kwa kujenga shule nyingi mpya za sekondari.

Anazitaja baadhi ya shule mpya kuwa ni pamoja na Sekondari Itende, Iziwa, Itangano na Nsalaga.

Hali kadhalika, anasema Rais Dk. Samia pia ameleta tabasamu Mbeya kwa kuleta Sh. bilioni 1.84 za Uviko ambazo zimejenga madarasa 92 ya shule za msingi.

Anasema kutokana na vitendo hivyo, yeye akiwa Mbunge na Spika baada ya kuona Rais amejenga madarasa, aliwaambia viongozi wa Jiji la Mbeya kwamba hataki kusikia shule inakosa vyoo na madawati.

Anasema yeye akiwa Mbunge, ameamua kuimarisha tabasamu la Rais Samia anayejenga shule nzuri maeneo mbalimbali kwa kuhakikisha watoto wote wanasoma huku wakiwa na vifaa muhimu.

Anasema wanafunzi 3,000 wanatoka kata zote 36 za Jiji la Mbeya kwenye kaya zenye kipato duni.

Anasema watoto hao wanapata vifaa hivyo na wataendelea kupata madaftari kadiri yatakavyokuwa yamejaa.

Dk. Tulia anawasihi wakazi wa Mbeya na Watanzania kwa jumla, kuwasaidia kwa hali na mali watu wasio na uwezo.

Spika wa Bunge anazungumzia pia kazi zinazofanyika jijini Mbeya kuwa ni ujenzi wa barabara kuu ya njia nne, na kwamba serikali pia imepanga kujenga barabara za mitaa 191 za jiji la Mbeya.

Aidha, inatarajia kuanza ujenzi wa soko la kisasa kwenye soko la zamani la Soko Matola na kwamba stendi kuu ya kisasa nayo itaanza kujengwa hivi karibuni.Kuhusu changamoto za umeme kukatikakatika, Dk. Tulia anawauliza wakazi wa Mbeya akisema mradi wa umeme Bwana la Mwalimu Nyerere, ni suluhisho la kero hiyo na kwamba tayari uzalishaji umeanza. \\Katika hafla hiyo iliyofanyika stendi ya daladala kabwe jijini Mbeya na kuhudhuriwa na watu mbalimbali.

Dk. Tulia anawasihi wakazi wa Mbeya kupokea tabasamu la Rais Samia kwa heshima.

Awali, baadhi ya viongozi waliohudhuria wakiwamo viongozi wa dini, machifu wakiongozwa na mzee Rocket Mwashinga, viongozi wa bodaboda, machinga, vyama vya siasa. Wafanyabiashara wananchi lukuki na madiwani wakiongozwa na mstahiki Meya Momamed Ally, walitoa kauli zao kuhusu Mbunge huyo na Rais Dk. Samia.

Mstahiki Meya anasema Mbunge Dk. Tulia aliwaelekeza viongozi wa Jiji kwamba shule zote ziwe na vyoo safi na kwamba hivi sasa vyoo 312 vinajengwa katika shule mbalimbali.

Anasema pia aliagiza shule zote ziwe na madawati na kwamba yametengenezwa 6,327 huku madarasa 54 yakikarabatiwa.

Anaongeza kuwa kutokana na ushauri wa mbunge huyo kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana, wametumia Sh. bilioni 3.8 kwa kuimarisha tabasamu sekta ya elimu na Mbeya wanapaswa kukumbuka deni la Rais Dk. Samia.

Viongozi wengine waliokuwepo ni maofisa elimu wa kata, maofisa mbalimbali wa serikali wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa.

Baadhi ya viongozi hao walipewa nafasi ya kuzungumza akiwamo Mwenyekiti wa waendesha bodaboda na bajaj Wilaya ya Mbeya, Alison Fwanda ambaye alimshukuru Mbunge Dk. Tulia kwa kuwakopesha pikipiki na bajaj zipatazo 400 na kwamba vijana wanaendelea kutabasamu kwa mikopo hiyo.

Anasema Dk. Tulia alianza kuwasaidia vijana kabla ya kupata ubunge na kwamba hivi sasa ameongeza kasi, jambo linaloonesha kuwa ni kiongozi aliyepania kuwasaidia watu wa Jiji na Mkoa wa Mbeya.

Mwenyekiti wa Wazee Jiji la Mbeya, Isakwisa Mwambulukutu, anasema tukio la kuwapatia wanafunzi 3,000 vifaa vya shule, ni la kwanza tangu Mkoa wa Mbeya uanzishwe.

Mwambukukutu alihudumu kwenye Chama Cha Mapinduzi (CCM) tangu enzi za Baba wa Taifa, Hayati Julius K Nyerere anasema kubwa zaidi Dk. Tulia ni wa kwanza pia kuongoza mmoja wa mihimili mikubwa nchini tangu mkoa uanzishwe.

Chifu Mkuu wa Jiji la Mbeya Rocket Mwashinga anasema Dk. Tulia ni kiongozi anayejitambulisha kwa kazi anazofanya zenye kujikita kwenye utu na ubinadamu.

Hafla hiyo ilihitimishwa kwa kuwakabidhi vifaa hivyo wanafunzi wachache wa mfano na kuelezwa kwamba walimu wakuu watavifuata katika Ofisi ya Mbunge.

Baadhi ya walimu wanasema tukio hilo liwe fundisho kwa wakazi wa beya wenye uwezo kifedha kuwasaidia wanafunzi wasio na viatu, sweta, madaftari na kwamba wengine hawana hata chakula nyumbani kwao wanakotoka.

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Januari 24 - 30, 2024 |




# Serikali hii inayofanya makubwa haichafuliki kitoto



UK. 12 & 13

Siasa



# Chadema mnahangaika bure, leteni sera mbadala

**Na Felix Lugeiyamu**

Mnamo tarehe 13 Januari, 2024, mwenyekiti wa chama cha upinzani, Chadema, Freeman Mbowe alitangaza maandamano kwa wafuasi wa chama chake nchi nzima.

Alidai ni maandamano ambayo yanalenga kushinikiza serikali kufuata maoni ya chama hicho (kwa mtazamo wangu). Nasema ni maoni ya chama kwa kuzingatia kauli ya mwenyekiti aliyoitoa. Nanukuu: "Kwa kuwa mapendekezo yetu yote yalionekana kukataliwa, chama kinatangaza maandamano ya amani ya kushinikiza serikali kuzingatia maoni na mapendekzo ya wadau mbalimbali wa uchguzi nchini ambayo yataanza Dar es Salaam tarehe 24 mwezi wa kwanza mwaka 2024 siku ya Jumatano (yaani leo) mpaka hapo serikali itakapoondoa miswada hiyo na kusikiliza na kuheshimu maoni ya wadau."

Kufuatia kauli hiyo wadau mbalimbali walijitokeza kupinga au kuunga mkono maandamano hayo yaliyotangazwa na chama hicho cha upinzani.

Muungano wa vyama vya upinzani zaidi ya 13 ulisema hawaungi mkono maandamano hayo na hivyo kufanya idadi ya wanaounga mkono maandamano hayo kupungua.

Kauli hiyo ya vyama pinzani ikanifanya nijiulize swali, hivi mwanasiasa huyu aliposema maoni ya wadau alimaanisha nini? Je, ni wananchi? Wanasiasa wapinzani kama yeye au ni mabeberu?

Kwa bahati mbaya sana wanaharakati wa vyama vingi vya upinzani hasa Afrika hupenda kutumia njia moja tu ya kutengeneza awareness na propaganda, nayo ni maandamano. Na siku zote lengo la maandamano huwa lina dhana mbili: ya kwanza ni kukataliwa na vyombo vya ulinzi na usalama na ikibidi kulazimisha ghasia ili ionekane kuna uvunjifu wa kile wanachoita demokrasia kwenye nchi husika.

Kama hii ndiyo njia pekee ya kufanya siasa katika nchi yetu basi tunahitaji kutafakari upya. Natambua kwamba siyo mara ya kwanzan kwa CHADEMA kuitisha maandamano lakini mara zote hawajawahi kuonesha kujifunza kwamba njii hii siyo sahihi kwa majira ya sasa yalivyo.

Akina Zitto Kabwe walipoandika Waraka wa Mabadiliko ukisababisha wafukuzwe Chadema, walisema njia ya hiyo maandamano na kile operesheni sijui sangara ni mbinu ya kisiasa iliyokuwa haikifikishi chama kokote.

Dhana ya pili ambayo wapinzani, hasa Afrika hupendelea ni ile ya kutengeneza chuki baina ya mtawala na mtawaliwa. Hii hutokana na matokeo ya maandamano yenyewe. Yaani kama likitokea baya basi mahubiri ya wanasiasa hawa huwa ni kuonesha wananchi kwamba serikali iliyo madakarani haifai kwa namna moja au nyingine na kwamba ni katili na siyo sikivu hata kidogo.

Ndugu msomaji, naomba ieleweke hakuna kitu kinakera katika nchi yetu na mataifa ya Afrika, kama kuendesha siasa za chuki baina ya wanasiasa wenzao ambao pia ni waafrika wenzao. Napenda sana maneno ya Kwame Nkuruah aliposema:

"Kama hatuwezi kuunda mipango kwa ajili ya umoja na kuchukua hatua madhubuti ili kuunda muungano wa kisiasa, hivi karibuni kutakuwa na vita ya wenyewe kwa wenyewe huku mabeberu na wakoloni wamesimama upande wa pili wa kioo na kuunganisha nyaya matata kutufanya kukatana makolomeo wenyewe kwa wenyewe kwa ajili ya malengo yao maovu barani Afrika." Maneno hayo alipata kuyanena January 7, 1961 alipokuwa akifunga mkutano huko Casablanca.

Tatizo langu hapa siyo kuwa mpinzani, bali jinsi tunavyotumia nafasi ya upinzani kama kijiwe cha kuendeshea mahitaji yetu binafsi ya kiu ya madaraka badala ya kuwaonesha wananchi sera mbadala.

Haiwezekani kuendesha siasa ya kuonewa huruma kila kukicha. Huu ni uchanga katika siasa. Niliguswa sana na maneno ya Dk. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi aliyoitoa hivi karibuni. Nanukuu: "Tunavyo vyama vya siasa nchini, tuendelee kushirikiana navyo. Milango ya ofisi yangu iko wazi. Wote tuna nia moja. Tutaendelea kushirikiana nao. Lakini kushirikiana nao haimaanishi kupunguza kasi ya kutafuta ushindi, kuongeza wabunge bungeni na madiwani, Serikali za Mitaa na ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi wa Rais mwakani.

Vyama vya siasa, wanasiasa na wadau wote wa maendeleo dhamira ya mazungumzo ni muhimu ikaakisi kote. Kukimbia na kukwepa mazungumzo sio ujasiri. Huo ni uoga. Hoja hujengwa kwa mdomo sio kwa miguu. Tunataka tuwapime kwa hoja zao, sio kwa miguu yao kuandamana. Vyama vya siasa vijitofautishe na mashindano ya urembo ambako hupimwa kwa jinsi wanavyotembea. Tutumie ubongo kufikiria, sio miguu."

Kimsingi kauli ya Dk. Nchimbi inafikirisha sana. Kwa msomi unahitaji kutambua kwamba hoja huzimwa na hoja lakini mwanariadha huzimwa na mwanariadha mwingine.

Kwa hatua nchi yetu ilipo haina uhitaji wa wanasiasa wanaoamini katika ghasia badala yake watengeneza hoja.

Hapo awali ilikuwa Chadema wakiitisha maandamano vyama pinzani vingine vilikuwa vinaunga mkono lakini safari hii vimepinga hatua hii tena kwa uwazi, je bado hatujifunzi?

Bahati mbaya kila mwanasiasa hutaja mwananchi kwenye mambo yake lakini huyu anayetajwa hapatagi nafasi ya kujisemea, laiti tungekuwa tunaruhusu wananchi wapate majukwaa kama ya wanasiasa watu wangekuwa wanaaibika kila uchao.

Ni wazi kwamba nchi yetu inaenda kwenye chaguzi za serikali za mitaa, inawezekana Chadema wana hofu ya kushindwa hata kabla ya uchaguzi na hivyo wanatafuta njia ya kuondoa utulivu wa wananchi katika kusikiliza hoja za wagombea kutoka chama tawala.

Ushauri wangu kwa Watanzania, wasiyumbishwe na siasa zilizopitwa na wakati badala yake wajikite kwenye kusikiliza hoja za wagombea na kufanya maamuzi sahihi.

Ushauri wangu kwa Chadema ni kurejea tena kuusoma Waraka wa Mabadiliko na kuufanyia kazi. Ulikuwa na hoja muhimu kwenu.

Hamisi Kibari
TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA
Simu: 0758143457

# Tusiache kuboresha Somo la Historia

KAMA nilielewa vyema, mwezi huu wanafunzi wa darasa la kwanza na la tatu wameanza mtaala mpya. Wale walioko darasa la pili watakutana na mtaala huo mwaka kesho wakifika darasa la tatu. Baadhi ya sekondari zilizochaguliwa kama za kuanzia, pia bila shaka zimeanza kutumia mtaala mpya kama nilimsikia vyema Waziri mwenye dhamana ya elimu nchini, Profesa Adolf Mkenda.

Ukiangalia vyema, mtaala mpya umezingatia kile alichokizungumzia na kukitaka Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, cha kuwa elimu ya kujitegemea hata kama utawala wake haukutekeleza vizuri dhana hii nzuri.

Mwalimu alitaka mwanafunzi anapohitimu kila ngazi fulani ya elimu awe na stadi fulani za maisha zinazoweza kumsaidia katika kujitegemea na hivyo asiendelee kuwa tegemezi. Yeye aliita upe. Leo takwimu za Tanzania, wategemezi ni wengi sana. Unaweza kukuta kwenye kaya, mtafuta mkate ni mmoja wategemezi sita!

Katika kutibu tatizo ka utegemezi, Mwalimu alikuja na shule za mchepuo wa kilimo, ufundi na biashara.

Lakini hapo katikati mambo yaliharibika kabisa. Hata hivyo, hizo shule maalumu za kilimo, kwa mfano sina hakika kama zilikuwa zinaendelea kufundisha kilimo. Angalau za biashara ziliendeleaendelea kidogo lakini masomo yale ya Bookkeeping (Utunzaji Mahesabu) na Commerce (Biashara) hayakuwa yakimjenga mtoto kufanya ujasiriamali labda kumwandaa kwenda chuo cha uhasibu ili akitoka huko atafute ajira.

Mtaala wa sasa unaonesha kwamba umejielekeza katika kutatua changamoto hiyo kwani wanafunzi wakimaliza elimu msingi itakayokuwa inaishia darasa la sita, wanaingia sekondari ambako, ama watakuwa kwenye mkondo wa amali au mkondo wa elimu ya jumla.

Katika mkondo wa amali, kadri nilivyoelewa mimi watoto watajifunza stadi mbalimbali; ujasiriamali, ufundi michundo, udereva, kilimo cha kisasa, uvuvi na kadhalika na kadhalika kiasi kwamba mtoto atakapohitimu elimu ya sekondari atakuwa sawa na mtoto atakayekuwa amesoma chuo cha ufundi (VETA).

Hii ni habari njema sana kwani inasemekana imewasaidia sana China kufika waliko sasa. Inaelezwa kwamba kutokana na vijana wengi wsa China kuwa na elimu ya ufundi, ilianza kwa kampuni za Ulaya na Marekani kupeleka teknolojia huko wakitafuta wafanyakazi wa malipo nafuu (Cheap Labor).

Waliichagua China kwa sababu vijana wao wengi walikua wamepitia 'Veta' za huko kwao kwa sababu kwa wale wa Ulaya na Marekani ni ghali kuwaajiri lakini mwisho wa siku China wakabaki na teknolojia na kuboresha zaidi. Sasa hivi ni namba mbili kwa uchumi wa juu, wakiifukuza Marekani ambayo bado inaongozaongoza! Zingatia neno 'inaongozaongoza'.

Inapendeza kusikia kwamba hata vijana watakaoingia mkondo wa elimu ya jumla ambako watasoma zaidi masomo haya yaliyozoeleka, hawataachwa hivihivi kwenye eneo la masomo ya amali. Watafundishwa pia lakini si kwa 'dozi' kubwa kama wale wenzao wa masomo ya amali.

Nimekuwa ninafuatilia na kugundua kwamba mtaala mpya pia umeboresha namna ya kujifunza masomo fulanifulani ikiwemo Kiswahili na Kiingereza.

Inawezekana sijapekua sana lakini nilidhamiria leo kuangalia suala la Somo la Historia. Inawezekana haya ninayoandika ni marudio lakini kama si marudio basi ni vyema yakafanyiwa kazi.

Pengine ingekuwa vyema kutoa mawazo kama haya wakati ule wa kukusanya maoni kwa ajili ya maandalizi ya huu mtaala mpya, lakini ninajua uandaaji wa mitaala ni jambo endelevu.

Kwa nini nimejikita kwenye Historia, ni kwa sababu ni kitu chenye umuhimu katika dhana nzima ya maisha ya mwanadamu. Kupitita historia, mtu huweza kutambua jana ilikuaje, leo ikoje na kesho iandaliweje.

Rais wa awamu ya tano, Mwendazake John Magufuli ninakumbuka pia aliwahi kuona umuhimu wa kuliangalia upya Somo la Historia akiamini kwamba likiboreshwa linaweza pia kuwasaidia vijana wetu kujenga uzalendo zaidi kwa taifa lao.

Mwandishi Felix Lugeiyamu ambaye kwa sasa analiandikia gazeti hili pia, alipata kuandika huko nyuma akishauri somo la Historia liangaliwe upya ili liendane na wakati.

Lugeiyamu aliandika: "Kitendo cha kusoma na kuiishi historia iliyoandikwa na mkoloni ni kuendelea kuishi na ukoloni na viashiria vyake vyenye lengo la kuendelea kumwonesha mwafrika kama kiumbe dhaifu kilichojaa unafiki, ulaghai na usaliti."

Lugeiyamu akaona kana kwamba historia inayofundishwa nchini ni kama inaonyesha kuwa watawala wa awali yaani machifu/watemi waliwasaliti waafrika wenzao kwa kuwauza wenzao utumwani kwa kuzuzuka na shanga na vitu vingine vidogovidogo.

Akauliza: "Ni kwa kiwango gani dhana hii ina ukweli? Ukiachilia mbali ukweli kwamba utumwa ulikuwepo hata kabla ya kuja kwa mkoloni, lakini je, ni kweli wazee wetu hawa waliopigania uhuru walikuwa wanawauza wenzao kwa kupewa shanga na vipande vidogo vya nguo? Ni nani awezaye kuthibitisha hili?"

Mwandishi huyo, akasema kwamba alipata bahati ya kutembelea vituo vya makumbusho ndani ya nchi yetu karibia mikoa yote, lakini kilichomshangaza na kumsikitisha, makumbusho aliyotembelea wakati huo takribani yote yalijaa vitu vya kutukuza ubeberu wa wakoloni kuliko uafrika!

"Utaona jinsi wanahistoria wanavyoeleza, namna mabeberu waliokuja kuharibu Afrika, kuliko kuelezea wazee wetu walioilinda Afrika kwa kila hali! Sasa huwa najiuliza vituo hivi vya makumbusho tumewaanzishia wakoloni au tumejianzishia?" Akajiuliza Lugeiyamu.

Ninachojaribu kusema hapa na kuungana na Lugeiyamu na kuangalia upya somo letu la Historia ili liangalie zaidi uafrika wetu, na husussani Watanzania tulikotoka kuliko wakoloni na kuona ni namna gani tunavyopaswa kuenenda.

Watoto wetu wawasome zaidi wanamapinduzi na mashujaa wa Afrika hata wa hivi karibuni kama akina Nelson Mandela, Kanali Muammar Gadafi, Julius Nyerere, Salim Ahmed Salum, Nkwame Nkrumah, Sajenti Samuel Doe, Robert Mugabe, Abeid Aman Karume, Dk. John Pombe Magufuli na wengine mfano wa hao.

Wawasome pia viongozi wa hovyo waliotaabisha wananchi wao badala ya kuwasaidia au kuongoza kwa mkono wa chuma au kuwa vibaraka wa wakoloni kama Iddi Amin Dada, Macias Nguema, Sani Abacha, Mobutu Seseseko na wengine.

Lakini tusiache kuwafundisha watoto wetu juu ya mashujaa waliopambana na wakolon kama Mkwawa, Milambo, Liti, Mangi Sina, Mangi Mery, Kinjekitile Ngware, Mwana Malundi na ngoma yake n.k.

Kwa mfano, Liti alikuwa mwanamama machachari pale Singida lakini unaweza kukuta mtoto wa Kinyaturu hafundishwi historia yake kwa mapana kulinganisha na na mawakala ukoloni kama Vasco Da Gama au Dk. Livingstone.

Masimulizi yanaonesha kwamba Liti alikuwa na uwezo wa kutumia nyuki kuwatimua wavamizi kwenye eneo laken n ahata wakoloni waliokwenda eneo lake walionja 'joto ya jiwe'!

Lakini wangapi wanajua kwamba kutokana na amani tulio nayo Tanzania ilianza kupokea wakimbizi hata kabla hatujapata uhuru? Ndiyo, kama huamini nenda kwenye shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na masuala ya wakimbizi la The Dignity Kwanza utapata majibu. Mambo kama haya na mengine lukuki ambayo kihistoria yanapatikana Tanzania au Afrika pekee watoto wetu wanapaswa kufundishwa.

Nadhani nimeeleweka.



**Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda akizungumza na wanafunzi**

Siasa

# Serikali hii inayofanya makubwa haichafuliki kitoto



**Na Hamid Yassin**

YALE maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) yaliyopangwa kufanyika nchi nzima kuanzia leo yamejifia kifo asilia kabla hata hayajafanyika baada ya kupingwa kila kona ikiwemo na vyama vya upinzani vyenyewe!

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe alitangaza Januari 13 kuwa, kuanzia Jumatano ya leo (Januari 24) watafanya maandamano ya 'amani' ya kupinga Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi na maisha magumu kwa Watanzania kabla ya Katibu wake Mkuu, John Mnyika kuibuka wiki iliyopita na kusisitiza maandamano hayo yapo na hakuna wa kuyazuia!

**KUTOUNGWA MKONO**

Wakati viongozi hao wa Chadema wakijinasibu hivyo, hali ni tafauti huko mitaani ambako watu na taasisi nyingi wameyapinga kwa kukaririwa kwamba hawatakuwa tayari kushiriki maandamano hayo yasiyo na tija wala mwelekeo.

Muungano wa vyama 13 vya siasa hapa nchini walikuwa wa kwanza kutoa tamko ya kuyapinga na kuwataka Watanzania wasishiriki maandamano hayo kwani wao wanataka kuvuna amani huku wakidai kuwa, viongozi wa Chadema wana dhamira ya kuivuruga nchi.

Viongozi wa vyama hivyo walikutana na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam Januari 17 na kutoa msimamo wao huo, huku Mwenyekiti wa umoja huo, Abdul Mluya akisisitiza kuwa, hoja zinazotolewa na Chadema kama sababu za kuandamana hazina msingi wala mashiko.

"Tunawaomba wananchi wasishiriki maandamano hayo na tunaitaka Chadema itoke hadharani kuwaomba radhi Watanzania kwa hatua hii walioamua kuichukua kwani inakinzana na utamaduni wetu," alisema Mluya.

Mluya aliongeza kuwa, kitendo hicho cha Chadema wanakichukulia kama ni ubinafsi wa kutaka kusikilizwa wao wakati nchi ina mfumo wa vyama vingi vinavyotambulika kisheria.

"Serikali isiwaogope wao, hicho ni chama kimoja lakini kinataka kupuuza mawazo ya wadau wengine waliotumia siku nyingi kutoa maoni katika kipindi ambacho wao awali waligoma kushiriki," aliweka wazi Mluya.

Wakati umoja huo wa vyama vya siasa wakiwapinga Chadema mchana kweupe, nao Watanzania waliohojiwa na vyombo mbalimbali vya habari kila pembe ya nchi wameweka wazi kwamba wamechoka kugeuzwa 'mbuzi wa kafara' na viongozi wa chama hicho wakirejea madhila makubwa waliyopata baada ya kushiriki maandamano ya huko nyuma ya chama hicho.

"Wanaandaa maandamano halafu wao viongozi waandamizi wa chama hicho hawajitokezi mstari wa mbele, matokeo yake sisi tunaofuata mkumbo ndiyo tunaoumia. Mimi binafsi hadi leo nina majeraha mwilini mwangu baada ya kushiriki maandamano ya mwaka 2010 kule Moshi Kilimanjaro ambayo watu zaidi ya watano walipoteza maisha," ameelezea kwa uchungu, Elieshi Tarimo mfanyabiashara wa mitumba Ilala Karume.

Mbali na wafanyabiashara mmoja mmoja kuyakataa maandamano hayo ya Chadema, lakini hata Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT) imeyapinga vikali kwa kile walichoeleza kuwa, mara nyingi waathirika wakubwa huwa ni wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao kando ya barabara na mitaani.

Mwenyekiti wa JWT, Hamis Livembe akizungumza na vyombo vya habari mkoani Lindi amewataka wanasiasa wenye hoja zinazotafautiana na Serikali kurudi kukaa mezani ili kupata suluhu badala ya kufanya maandamano.

"Wafanyabiashara tunapinga haya maandamano kwa sababu sisi ndiyo waathirika wakubwa kwa kuwa huwa yanapita sehemu zetu za biashara na wao wanapenda kupita sehemu zenye biashara na mikusanyiko ya watu wengi, rabsha zinapozidi maduka hufungwa , yanavunjwa na siku hiyo biashara haziwezi kufanyika, kwa hiyo sisi tunapinga jambo hili,' amesema Livembe

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imefanya mengi mazuri katika kipindi hiki inachoelekea mwaka wake wa tatu, na itakuwa ni uzandiki wa hali ya juu kuanza kutamka kwamba imevurunda kiasi cha kuanza kuipaka matope mbele ya Watanzania.

Pia ifike mahali ieleweke kuwa, upinzani si kukosoa kila kitu. Yaani Mbowe hayaoni mazuri au mipango mizuri inayofanywa na serikali hii ya awamu ya sita kwa faida ya wananchi wake?

**AWAMU YA SITA MOTO**

CCM na uongozi wa awamu zake zote sita tangu taifa hili lipate uhuru inatimiza majukumu yake kupitia Ilani zake za uchaguzi inazoziweka sambamba na kufuata matakwa ya katiba na taratibu za nchi na si matamko ya taasisi, vyama vya siasa ama watu binafsi.

Ni mwendo wa kupokezana kijiti kutekeleza yote yaliyoahidiwa na chama chao kuanzia serikali zilizopita, ya sasa na zile zitakazofuata na wala sio kama pale Chadema atakachoamua Mbowe hata kiwe na walakini kiasi gani akina Mnyika na wenzake wanaishia kusema; "Ndiyo Mzee!"

Ndiyo maana Serikali ya awamu ya sita ilishaweka hadharani kuendeleza mipango yote ya awamu zilizotangulia ambayo aidha bado inatekelezwa ama ipo mbioni kutekelezwa; kama vile ujenzi wa reli ya kisasa toka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma.

Pia kukamilisha ujenzi gati Bandari ya Mtwara, kuendeleza ujenzi wa daraja kubwa la Busisi kule Mwanza, imeshakamilisha ujenzi wa daraja la Salender (Ocean Road Sea Bridge), pia vivuko kadhaa vinajengwa kwenye mikoa mbalimbali nchini zikiwemo meli na pantoni.

Awamu hii pia imeshaweka

**Siasa**



Chuo Kikuu cha Dodoma


hadharani kuendeleza ujenzi wa barabara ya njia sita kutoka Dar es Salaam hadi Chalinze mkoani Pwani. Ujenzi wa viwanja kadhaa vya ndege ikiwemo kumaliza huu mkubwa wa Dar na mikoani ambapo miradi hiyo ilianzia tangu awamu zilizotangulia.

Kuna miradi mikubwa ya maji kote nchini sambamba na ile ya umeme kama ule wa Bwawa la Julius Nyerere ambao uzalishaji wa umeme uko mbioni kuingizwa kwenye gridi ya taifa na kuwaondolea Watanzania adha ya muda mrefu ya umeme wa mgawo.

Ule mradi mkubwa wa ujenzi utakaotoa ajira kubwa kwa Watanzania wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Tanga, Serikali ya awamu ya sita inaendelea kuusimamia kikamilifu kwa kushirikiana na Serikali ya Uganda.

Pia kuna mradi mwingine mkubwa wa matumizi ya gesi kule Mtwara, mradi mkubwa wa kusambaza maji Dar es Salaam yote, mradi wa ujenzi wa barabara za mwendo kasi sehemu kubwa ya Dar es Salaam (BRT) sasa upo katika awamu ya nne.

Ununuzi wa ndege za ATCL unaendelea ambapo ndani ya mwaka huu 2024 zitapokewa ndege mbili ikiwemo nyingine ya mazigo, ujenzi wa Barabara ya Mawasiliano kiwango cha lami. Ujenzi wa Kituo cha Pamoja bandarini (One Stop Centre), ufungaji wa Scanner bandari za Dar na Tanga, mradi wa umeme vijijini (REA) na ujenzi Bandari Kavu Ruvu inaendelezwa kwa kasi kubwa tangu ianzishwe na serikali ya Awamu ya Tano.



SGR

Kuna rafiki yangu mmoja kada na kiongozi wa CCM, Mpiganaji Songoro Hamis Mnyone huwa anasema kuwa, mtu yeyote yule aliye na mafanikio leo ni kwa sababu ya CCM, yeyote aliye na elimu leo ni mafanikio ya CCM, yeyote aliyoko DP, CUF, UDP, CHADEMA, TLP, ACT ni mafanikio ya CCM. Nami ninathibitisha haya kama ifuatavyo.

**MAENDELEO YA BARABARA**

Barabara za lami, kipindi nchi yetu inapata Uhuru mwaka 1961 kulikuwa na miji mitano pekee iliyokuwa na vipande vya lami ambavyo vilikuwa havizidi kilomita 1,200, kumbuka wakoloni walitawala Tanganyika miaka 75 lakini wakashindwa kujenga barabara za lami wakati CCM imeongoza Tanzania miaka 63 imeunganisha nchi nzima kwa barabara ya lami.

Mpaka sasa kuna zaidi ya kilometa elfu 16 zilizojengwa kwa kiwango cha lami, zamani ilikuwa kutoka Dar mpaka Mwanza ni siku kadhaa, leo ni masaa 16 pekee.

Zamani, wakati nchi inapata uhuru, kutoka Dar mpaka Bukoba ilikuwa siku zaidi ya saba leo ni siku mbili tu safari ya umbali wa zaidi ya kilometa 1500, kutoka Dar hadi Sumbawanga ilikuwa siku saba, leo ni saa 17.

Kwa ujumla mikoa yote imeunganishwa kwa barabara za lami ambazo nyingi zilianza kujengwa kwa kasi tangu awamu ya tatu na kuendelea kuendelezwa wakati huu wa awamu ya sita chini ya Dk. Samia jambo linalorahisisha ukuaji wa uchumi.

**ELIMU YA JUU**

Elimu ya juu, nchi yetu wakati inapata Uhuru kulikuwa hakuna chuo kikuu Tanganyika na Afrika Mashariki kulikuwa na Chuo Kikuu kimoja tu ambacho ni Makelele cha Uganda, lakini leo ndugu msomaji kuna vyuo vikuu zaidi ya 62 vya serikali na binafsi.

Takribani kila mkoa kwa sasa una chuo kama sio cha kati au cha ufundi basi chuo kikuu. Mkoa wa Dar es salaam pekee una vyuo vikuu 34 na hayo yote ni mafanikio ya serikali ya inayoongozwa na CCM.

Kwa upande wa elimu ya msingi na sekondari, kabla ya Uhuru elimu ya nchi yetu ilikuwa ya kibaguzi watoto wa machifu ndio waliokuwa wakipewa kipaumbele kusoma ili waendelee kuwa watawala.

Wakati huo kulikuwa hakuna elimu ya 'A level', lakini mwaka 1965 serikali ikafanya mapinduzi makubwa katika mfumo wa elimu kwa kuanzisha darasa la kwanza mpaka la saba, kidato cha kwanza mpaka cha nne na kidato cha tano hadi cha sita pia mwaka huo serikali ikataifisha shule zote za wamissionari na kuziweka serikali na miongoni mwa hizi shule ni pamoja na Tosamaganga, Milambo, Nsumba, Minaki, Mpwapwa na nyingine nyingi.

Shule za msingi zimeongezeka sana, karibu kila kijiji sasa kina shule; mwaka 2007 serikali ikajenga shule za kata kote nchini, na hivi sasa serikali imetangaza elimu ya shule ya msingi hadi kidato cha nne kuwa ya lazima ili kuongeza uelewa kwa Watanzania wote.

**UHURU WA KUPATA HABARI**

Vyombo vya Habari, ndugu zangu kama wewe sio mnafiki utakubaliana na mimi kuwa katika swala la Uhuru wa vyombo vya habari Tanzania imepiga hatua kubwa sana na inapaswa kuigwa, nchi yetu kwa sasa ina zaidi ya vituo vya redio 123 na televisheni 36 na magazeti zaidi ya 200 ya serikali na watu binafsi.

Kabla ya Uhuru kulikuwa hakuna redio za binafsi na TV kama ilivyo sasa haya yote ni maendeleo ya hali ya juu.

**MAWASILIANO**

Matumizi ya simu na mitandao wakati tunapata Uhuru hayakuwepo kwani masafa hayo ya mtandao kipindi cha wakoloni simu zilitumiwa na wamissionari pamoja na maeneo yenye vyombo vya ulinzi na usalama, lakini leo kuna Watanzania zaidi ya milioni 20 wanaotumia simu za mkononi, kila ofisi ina simu za ofisini, kuna mitandao ya mawasiliano kila jiji, miji na manispaa; kwa sasa mtoto wa miaka sita anajua kutumia simu.

Wakati nchi yetu inapata uhuru huduma za posta zilikuwepo zilizoanzishwa mwaka 1880 na Wajerumani na zilikuwa zinapatikana maeneo yaliyokuwa na watawala wa kikoloni tu, ilikuwa mwananchi akihitaji huduma hii anatumia siku mbili kuifuata lakini leo kila sehemu ina ofisi za posta na EMS vitu vinavyo rahisisha ufikishwaji wa barua.

**UMEME**

Kwa upande wa ishati ya umeme, kwa wale watu wazima watakumbuka na kwa wale vijana hususani mnaopenda kusoma vitabu vya historia ya nchi yetu mtakubaliana nami, kipindi tunapata Uhuru mikoa michache sana ilikuwa na umeme na hata ile iliyokuwa na umeme ulikuwa baadhi ya maeneo ya katikati ya mji na mikoa iliyokuwa na umeme haifiki hata 10.

Kwa sasa mikoa yote nchini ina umeme na sasa serikali inasambaza umeme vijiji vyote nchini kupitia Wakala wa Umeme Vijini (REA) ili kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa na umeme, lakini pia serikali imepunguza gharama za manunuzi ya umeme na kuunganisha mitambo ya umeme majumbani kwa kutumia mashine mpya.

**USAFIRI WA ANGA**

Usafiri wa Anga, kabla ya Uhuru nchi yetu ilikuwa na viwanja vya ndege takribani viwili vilivyokuwa vinatambulika lakini kwa sasa nchi yetu ina viwanja vikubwa vya kimataifa vinne ambavyo ni; KIA, Songwe, Mwanza na Kwanja cha Ndege Kimataifa cha Julius Nyerere.

**HUDUMA ZA AFYA**

Huduma ya Afya, kabla ya Uhuru zilikuwa duni sana. Akina mama wengi walikufa kipindi cha kujifungua, lakini sasa takribani kila kijiji kina kituo cha afya, hospitali za rufaa zimeongezeka sana karibu kila kanda ina hospitali ya rufaa, mfano hospitali ya rufaa ya Mbeya, Moshi, Bugando Mwanza na hospitali ya Taifa Muhimbili.

Kwa sasa kila Mkoa una hospitali ya Mkoa na kila Wilaya pia, serikali ya CCM imeanzisha utaratibu kwa sasa mama wajawazito wanatibiwa bure, wazee na watoto, serikali ya awamu ya sita imerahisisha upatikanaji wa dawa na kurahisisha bei na sasa kuna utaratibu wa kuunganisha Watanzania wote na huduma za bima ya afya sasa ni lazima.

Haya yote yamefanywa na CCM kuanzia awamu yake ya kwanza chini ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hadi hii ya sita ya Dk. Samia Suluhu Hasaan.

Kwa mtaji huu, Mbowe na wenzake wanaweza kweli kuichafua Serikali ya CCM au kuzima kasi hii ya maendeleo kwa maandamano ya ujanjaujanja?

Ni vyema wajiandae na operesheni 'safisha' Jiji ya Albert Chalamila. Yaani ameahidi takataka zote zitakazozolewa huko mitaani zitasombwa kwenye magari maalumu tayari kwa kwenda kutupwa kwenye madampo!

*Kwa mawasiliano Mwandishi wa makala haya; 0784 122020 na 0768 888787.*

Siasa

# Waliosemwa wamechoka 2013, 2024 bado wapo Chadema

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA 11 iliyopita, yaani mwaka 2013, waraka wa Mkakati wa Mabadiliko ulivuja na kusambaa mitandaoni, hatua iliyosababisha baadhi ya viongozi waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuondolewa wakituhumiwa kuandaa mkakati huo.

Ulikuwa ni mkakati uliohitaji kufanyika kwa mabadiliko ya haraka ndani ya chama hicho kwa kile kilichoelezwa kwamba ni kuchoka na kukosa mbinu kwa uongozi uliokuwa madarakani wakati huo.

Kwa kutumia mifano ya matukio mbalimbali, mkakati ulionesha kwamba chama hicho kilihitaji kuhuishwa haraka kwa kuja na damu mpya ya uongozi kwani mbinu za maandamano na harakati nyingine hazikuonekana kukisaidia chama hicho kikuu cha upinzani nchini kuvuna wafuasi wengi na hata kushinda chaguzi mbalimbali.

Baadhi ya waliofukuzwa baada ya mkakati huo kuvuja ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Zitto Kabwe (sasa kiongozi wa ACT-Wazelendo), aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema Profesa Kitila Mkumbo (sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji) na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Arusha, Samsoni Mwigamba.

Sasa ikiwa ni takribani miaka 11, tangu mkakati huo upangwe na kuonesha mapungufu ya uongozi, bado viongozi waliodaiwa kuchoka na kukosa mbinu ndio bado wanaongoza Chadema.

Uongozi huo umekuwa ukidai eti serikali ya chama tawala inanyima demokrasia wakati wenyewe ndio unadaiwa kuwa kinara wa udikteta. Yaani unaona kibanzi kwenye jicho la jirani wakati wenyewe una boriti jichoni.

Wengi walitazamia kwamba, mbali na hatua ambazo Chadema ilichukua dhidi ya wana mapinduzi walioona kuna haja ya kufanya mabadiliko ya uongozi, basi viongozi wa sasa wangeutumia waraka huo kama kioo na kubadilika lakini wanarudi kulekule.

Safari hii wamekuja tena na mbinu za maandamano zilizoelezwa kwenye mkakati huo kwamba zimepitwa na wakati na hazina tija. Tujikumbusha yaliyokuwemo kwenye huo waraka.

**UTANGULIZI:**

Taasisi tunayoizungumzia ilisajiliwa rasmi mwezi January 1993 na tokea wakati huo imeongozwa na wakuu wa taasisi wapatao wawili na aliyepo kwa sasa ni wa tatu.

Wa kwanza aliongoza kwa miaka mitano tangu wakati huo 1993 hadi 1998 na kumwachia aliyefuata ambaye naye aliongoza kwa miaka mitano hadi mwanzoni mwa 2004 na kumwachia aliyepo sasa.

Huyu aliyepo aliongoza kwa miaka mitano tangu mwaka 2004 hadi 2009 na kisha akachaguliwa tena mwaka 2009 kwa kipindi cha pili. Tunapenda kwa hatua ya mwanzo kabisa kutambua juhudi za wakuu wetu wote waliopita walizozifanya katika kuhakikisha taasisi yetu inakua kwa kutumia uwezo wote waliokuwa nao na katika mazingira yaliyowakabili.

**WAWAKILISHI BUBGENI**

Mwaka 1995 chini ya mkuu wa kwanza tulipata wawakilishi watatu kwenye chombo chetu kikuu cha uwakilishi. Mwaka 2000 chini ya mkuu wa pili tukapata wawakilishi wanne pamoja na wa nyongeza mmoja na kufanya idadi kuwa watano. Mwaka 2005 chini ya mkuu wa tatu ambaye ndiye aliyepo hivi sasa, tulipata wawakilishi watano na wa nyongeza sita jumla wakawa 11.

Mwaka 2010 chini ya mkuu huyu huyu wawakilishi wakaongezeka na kuwa 23 na wa nyongeza 25 na kufanya idadi kuwa 48 kabla ya kupata mwingine mwaka jana na kufanya sasa wawe 49.

**WAASISI HAWAKUWA MADIKTETA**

Tunapopongeza juhudi zao hizi tunahitaji pia kuwapongeza wakuu wetu wawili wa kwanza ambao kimsingi waliweka msingi mzuri sana wa kutong'ang'ania madaraka na badala yake kuachia mapema na kumwachia mwingine kidemokrasia bila vurugu.

Hawakuwa madikteta na tunawapongeza sana. Walijitahidi sana kutokuwa wapenda madaraka na kimsingi walituwekea utamaduni ambao walitaka wote tuufuate na kujenga taasisi imara inayojali demokrasia na haki ya kila mwana taasisi.

Ni kwa msingi huo waliamua kuandika kabisa katika mwongozo wetu kwamba kiongozi yeyote katika ngazi yoyote ya kuchaguliwa atakapogombea na kushinda ataongoza kwa kipindi kimoja cha miaka mitano na kisha ataweza kugombea na kuongoza kwa kipindi cha pili cha miaka mitano baada yapo hawezi kugombea tena katika nafasi ile ile aliyoitumikia kwa vipindi viwili.

Ili kuonesha kwamba walimaanisha kile walichokisema, wote wawili hawakuwahi kukaa madarakani kwa vipindi viwili vilivyoruhusiwa katika mwongozo bali wote wawili walikaa kipindi kimoja kimoja tu.

**SASA (2013) NI SHIDA**

Lakini kuna matatizo yameanza kujitokeza na tusipochukua hatua haraka huko mbele tunaweza kupata shida kubwa. Tunapenda kuainisha matatizo hayo kwa uchache kama ifuatavyo:

Wakati tukiufanyia mwongozo wetu mabadiliko mwaka 2006 hatukugusa kipengele kinachomzuia kiongozi kuongoza kwenye nafasi moja kwa zaidi ya vipindi viwili vya miaka mitano mitano.

Lakini wakati mwongozo unachapwa chini ya uongozi uliopo, kipengele hicho kiliondolewa kinyemela. Mambo yanayotokea hivi leo yanaonyesha dhahiri kipengele hicho kiliondolewa kwa makusudi kwa maslahi na kwa faida ya viongozi waliopo madarakani kwa sasa.

Hiki kinaweza kuchukuliwa kama kitendo kidogo lakini kama viongozi wetu wanaweza kutokuwa waaminifu katika jambo kama hili, ni dhahiri hawawezi kuaminika na wanaweza kufanya mambo mengine makubwa na yenye athari zisizomithirika kwa taasisi yetu.

**UONGOZI UMEISHIWA MBINU**

Ni dhahiri kwamba uongozi uliopo umeishiwa mbinu na kuakisi jambo la msingi sana ambalo waasisi wetu waliliona tangu mwanzo na kuamua kuweka kipengele cha ukomo wa uongozi kwenye mwongozo wetu.

Kuchoka kwa uongozi wetu kunaonekana dhahiri katika mipango na mikakati ya taasisi ya miaka kadhaa. Mfano mwaka 2008 uongozi ulianzisha mkakati wa operesheni samaki mkubwa (maarufu kama Operesheni Sangara).

Huo ulifanyiwa kazi katika mikoa kadhaa na hatimaye ikafa kimya kimya. Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 kulianzishwa matembezi ya maandamano ambayo nayo yalikuwa yakipeleka ujumbe kwa watu na yalipangwa kufanyika mikoa yote na wilaya zote.

Kumbukumbu zetu zinaonyesha kwamba yalikuwa yakianzia makao makuu ya mkoa na kwenda kwenye wilaya zote. Lakini kumbukumbu hizo zinaonyesha kwamba yalifanyika Mwanza, Musoma, Shinyanga, Kagera na mikoa ya Nyanda za Juu kusini (Mbeya, Iringa, Njombe na Rukwa) kisha nayo yakafa kifo cha mende. Kisha mwaka 2012 ikaanzishwa operation ya mabadiliko maarufu kama Movement for Change (M4C).

Hiyo ilikuwa inakwenda kwenye mikoa na timu kama nne hivi ambazo kwa ujumla zilitathmini hali ya mtandao na uongozi wa taasisi, kuhamasisha umma kwa njia ya mikutano ya hadhara, kuingiza wanachama na kusimika uongozi na hatimaye kufanya mafunzo kwa viongozi.

Hiyo ikafanyika Mtwara na Lindi, Morogoro na kisha ikaenda kufia Iringa. Mwaka huu (2013) viongozi wetu wamekuja na ugatuaji madaraka kutoka makao makuu ya taasisi na kupeleka madaraka kwenye kanda mbalimbali.

Mkakati huu ulikufa kabla ya kuanza pale viongozi wakuu walipobadilisha maazimio ya kikao kikuu na kutekeleza matakwa yao ikiwa ni pamoja na kuleta suala la viongozi wa muda kwa muda mrefu badala ya kuajiri maofisa na wakahakikisha wanaweka watu wao kwenye uongozi wa muda.

Kitendo hiki kwa peke yake, cha kufeli kwa kila mkakati unaoletwa na viongozi wetu katika hatua za utekelezaji unaofanywa na wao wenyewe waleta mkakati, ni kiashiria tosha kwamba uongozi uliopo umechoka.

**HATUTOBOI KWENYE CHAGUZI**

Performance yetu kwenye chaguzi ndogo nayo ni ishara kwamba mabadiliko yanahitajika. Tangu uongozi huu uingie madarakani, kumefanyika chaguzi ndogo 8 za wawakilishi kwenye chombo kikuu, kati ya hizo tumeshinda 2 tu sawa na asilimia 25 (hadi kufikia mwaka 2013). Aidha baada ya mwaka 2010 kumefanyika chaguzi kadhaa za wawakilishi kwenye halmashauri.

Mwezi Oktoba 2011, mwezi wa4 2012, mwezi Septemba 2012 na mwezi Juni 2013. Kote performance yetu imekuwa poor kupindukia. Mfano mwezi wa Juni 2013 tumepata viti 6 kati ya 22 (asilimia 27) na mwezi Septemba 2012 tulipata viti saba kati ya 29 (asilimia 24).

Ni dhahiri mabadiliko yanahitajika kwa kuwa wakuu waliopo wanatumia mbinu zile zile na kupata matokeo yale yale. Tunahitaji mbinu mpya. Kwa kifupi, ushindi ambao tumekuwa tukiupata katika chaguzi ndogo haulingani na ukubwa wa hamasa kwa taasisi yetu iliyopo mitaani.

Hii ni kwa sababu tumekuwa tukitumia mbinu hizohizo katika kila chaguzi. Aidha, tu wepesi mno wa kuridhika na kujisifu kwa mafanikio madogo badala ya kukaa chini na kutafakari kwa kina mahala tunapojikwaa.

Itandelea



**Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa Chadema akihutubia katika moja ya mikutano ya chama hicho. Mbowe amekuwa kiongozi mkuu wa Chadema tangu mwaka 2004.**

# Ujue ugonjwa unaosababisha macho kutoka nje

MAGONJWA ya tezi ya macho, ni ugonjwa wa kawaida zaidi kwa wanawake, lakini huwa mbaya zaidi kwa wanaume.

Katika shingo, kuna tezi yenye umbo la kipepeo (thyroid) yenye aina mbili za homoni - T3 na T4 . Tezi hii huamua jinsi viungo tofauti vya mwili vinavyofanya kazi haraka.

Lakini wakati kuna hitilafu katika tezi hii, homoni iliyotengenezwa na ubongo ambayo hutuma amri kwa tezi kufanya kazi, mwili unaweza kupata majeraha.

Mtu anapopatwa na maradhi haya, huanza kupungua kwa uzani wa mwili, kuvimbiwa, matatizo ya kumbukumbu, uchovu mwingi, hedhi isiyo ya kawaida, kupungua kwa kasi ya mapigo ya moyo na kupotea kwa nywele.

Hata hivyo, wakati T3 na T4 zinazalishwa kupita kiasi, mtu hupata baadhi ya usumbufu ikiwemo kama vile mapigo ya kasi ya moyo, wasiwasi, kutokwa na jasho na hata kutetemeka kwa mwili.

Lakini kuna athari ya nadra ambayo haijajulikana sana kuhusiana na hali hii inayohusishwa kitendo cha tezi kuzalisha homoni kupita kiasi hali inayojulikana na kama hyperthyroidism, hali ambayo inaweza kuwa na matokeo mabaya juu ya afya na ubora wa maisha. Miongoni mwa athari hizi ni ugonjwa wa tezi ya macho ambao pia unajulikana kama orbitopathy ya Graves au ophthalmopathy.

Katika hali hii, uvimbe ambao unajitokeza nyumba tundu la jicho husukuma macho mbele na kusababisha usumbufu unaosababisha kupoteza uwezo wa kuona.

Habari njema ni kwamba kuna njia za kutibu hali hiyo na wataalam kutoka Ulaya na Marekani hivi karibuni, waliungana pamoja kufafanua njia bora za kupambana na ugonjwa huu. Katika miezi ya hivi karibuni, dawa mpya maalum dhidi ya ugonjwa wa orbitopathy ya Graves, pia imeidhinishwa nchini Brazil.

Daktari wa wa macho, Stefânia Diniz, mtaalamu wa oculoplasty au kitengo kinachohusika na matibabu ya kope, ducts za machozi na uso, anakadiria kuwa karibu asilimia 30 ya wagonjwa walio na kiwango kikubwa cha uzalishwaji wa homoni kupita kiasi huwa na uwezekano mkubwa wa kupata ugonjwa wa jicho la tezi.

Uchunguzi wa kimataifa unaonyesha kuwa ugonjwa huu huathiri kati ya asilimia 0.5 na mbili ya idadi ya watu duniani.

Kwa hiyo, hesabu ya msingi inabainisha kuwa uzalishaji wa T3 na T4, huathiri Wabrazil kati ya milioni moja na milioni nne na miongoni mwao, 300,000 hadi milioni 1.2, pia wanakabiliwa na ugonjwa wa tezi ya macho.

Ikumbukwe kwamba takwimu hizi ni makadirio tu, kwani hakuna tafiti maalum zilizochapishwa juu ya suala hili nchini.

"Ni ugonjwa ambao unaweza kujidhihirisha kupitia dalili kali na zisizo maalum, kama vile ukavu au wekundu wa jicho, hadi usumbufu mkubwa ambao unaathiri uwezo wa kuona," anaelezea Dk. Diniz.

"Kwa bahati mbaya, ugonjwa wa macho ya tezi, huchelewa kugundulika kwa sababu ya ukosefu wa maarifa juu yake miongoni mwa watu wengi na miongoni mwa madaktari," analalamika mtaalamu.

Lakini baada ya yote, tatizo linaloathiri tezi linaweza kuwa na athari katika eneo maalum kama nyuma ya jicho?

**Tezi lenye umbo la kipepeo iliyoko shingoni inawajibika kuzalisha homoni T3 na T4**

Ni muhimu kuelezea kwamba ugonjwa wa jicho la tezi ni ugonjwa wa autoimmune.

Kwa maneno mengine, hii inamaanisha kuwa vitu vinavyozalishwa na mfumo wa ulinzi yenyewe, huanza kushambulia sehemu maalum za mwili.

Katika hali hii , antibodies (protini zinazoukinga mwili kushambuliwa) fulani huharibu kazi ya macho.

"Seli zilizoathirika huanza kuzalisha vitu vinavyoitwa glycosamines, ambavyo huvutia maji. Hii kwa upande wake huunda uvimbe ambao husababisha jicho kuwa kubwa na kutoka mbele ," anafafanua.

"Baada ya muda, seli hizi zinaweza kutofautisha na kuzalisha tishu zaidi za adipose (mafuta) au misuli katika eneo hilo," daktari anaongeza.

Kwa maneno mengine, eneo la obiti ya macho ambalo tayari ni la kawaida, linakusanya vitu vingi ambavyo havipaswi kuwa hapo.

Idadi kubwa ya visa vya ugonjwa huu wa macho zinahusishwa na utengenezwaji wa ziada wa homoni.

Lakini baadhi ya wagonjwa hupata ugonjwa huo, hata kutokana na tezi yenye afya.

Katika hali mbaya zaidi, macho huvimba au hata kupoteza uratibu wa harakati (kile kinachoitwa strabismus katika duru za matibabu). Baadhi ya wagonjwa wanakabiliwa tatizo la kuona vitu mara mbili mbili au hata hushindwa kabisa kufunga tena kope zao.

Villagelin inakadiria kuwa asilimia 80 ya wagonjwa wana aina kali zaidi za ugonjwa wa macho ya tezi, huwa na dalili za kuwasha au wekundu wa macho huhisi kana kwamba wana mchanga ndani ya macho yao.

Lakini tunawezaje kuzuia tatizo kama hili kufikia hatua kali zaidi?

**Sehemu yeye tundu ambapo jicho linafaa kuwa ni ndogo na linatoa uvimbe na makovu kwa watu wenye ugonjwa wa tezi ya macho.**

Dk. Diniz anasema kuwa ugonjwa wa jicho la tezi umegawanywa katika awamu mbili tofauti, unaotibika na sugu.

Wakati wa matibabu ya ugonjwa unaotibika ambayo kwa ujumla huchukua kati ya miezi sita na 18, mchakato wa uchochezi unaendelea na usumbufu unaendelea kidogo kidogo. Lakini katika hali ya ugonjwa kuwa sugu, tishu zilizokusanywa huanza kuunda makovu.

"Ugonjwa sugu au wenye makovu, ni mgumu zaidi kuutibu, kwa hiyo kadiri ugonjwa unavyogundulika mapema, huweza kutibika, " anasema.

Daktari wa ophthalmologist pia anasisitiza kuwa utambuzi unaweza kufanywa ofisini, kupitia uchunguzi wa dalili na ripoti ya mgonjwa wakati mwingine wataalamu huagiza mgonjwa afanyiwe uchunguzi wa maabara au vipimo vya picha ili kuondoa sababu nyingine za matatizo katika eneo hilo, kama vile uvimbe.

Mara tu ugonjwa wa tezi la jicho unapogunduliwa, matibabu yanaweza kuanza ambayo yatatofautiana kulingana na ukali wake.

Sgarbi na Villagelin, wanasema kuwa hatua ya kwanza ni kuimarisha utengenezwaji wa homoni katika tezi na dawa ambazo husaidia kudhibiti uzalishaji wa homoni ya tezi.

"Mwongozo wa pili ni kumuomba mgonjwa aache kuvuta sigara, kama inawezekana," anaongeza Villagelin.

Utafiti uliochapishwa katika miongo kadhaa iliyopita umegundua kuwa utabiri wa ugonjwa wa tezi la jicho ni mbaya zaidi kwa wavutaji sigara.

Sababu bado hazijajulikana kwa uhakika, lakini madaktari wanashuku kuwa sigara huongeza hali ya uchochezi wa mwili, ambayo ina athari kwenye tundu la jicho.

Pia kuna matibabu maalum ya kutibu ugonjwa wa orbitopathy yenyewe. Baadhi ya matone ya jicho na vilainishi vya macho husaidia kulainisha macho na kupunguza usumbufu wa haraka, kama vile kuwasha kunakosababishwa na ugumu wa kufunga kope.


"Kulingana na ukali, tunaweza kutumia dawa za kupambana na homoni za ziada, kupitia tiba ya mionzi au kufanyiwa upasuaji," anasema Dk. Diniz.

Lengo ni hasa kuacha uvimbaji wa jicho na kuongezeka kwa kaboni ambayo hujilimbikiza katika sehemu ya ndani ya jicho.

Katika hali kama hii, upasuaji wa tishu zilizokusanywa hufanyika ili kuziondoa kupunguza shinikizo na kurekebisha kasoro za jicho.

BBC.









> Lakini kuna athari ya nadra ambayo haijajulikana sana kuhusiana na hali hii inayohusishwa kitendo cha tezi kuzalisha homoni kupita kiasi hali inayojulikana na kama hyperthyroidism, hali ambayo inaweza kuwa na matokeo mabaya juu ya afya na ubora wa maisha.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462



# Msingi wa maadili mema huanzia nyumbani

KWA mujibu wa mtandao wa Wikipedia; maadili ni mafundisho yanayotolewa katika nafasi mbalimbali, hasa katika malezi, ili kuelekeza binadamu atende namna ambayo inamjenga yeye na jamii nzima. Maadili yanajumuisha kanuni na imani zinazokubaliwa katika jamii.

Kwa lugha nyingine matendo yote yasiyokubalika katika jamii kama hii yetu ya Kitanzania yanapofanywa na mtu ni kwenda kinyume na maadili.

Matendo ya hovyo yako mengi, hii ni kuanzia mabaya zaidi na hatari (uhalifu) kama mauaji, ujambazi, ushoga na ubakaji hadi yanayoanza kuzoeleka katika jamii kama kula rushwa, wizi wa mali ya umma, ulevi wa kupindukia, kukosa heshima, kuvaa nusu uchi, kutukana, kubagua au kunyayasa wengine, kusengenya, kusema uongo na kadhalika.

Si jambo la kuficha kusema tunaishi katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa maadili yamemomonyoka sana na yanaendelea kumomonyoka.

Kwa kuwa mimi ni mdau wa malezi na maadili kutokana na kuwa mwalimu kwa taaluma, nitaendelea kuzungumzia sana maadili na malezi.

Hata hivyo, mmomonyoko huu wa maadili si tu upo kwa baadhi ya watoto na vijana, lakini pia hata baadhi ya wazazi na walezi, ambapo kimsingi wazazi na walezi ndiyo walipaswa kuwa kielelezo kizuri cha kuwalea watoto katika misingi ya maadili mazuri.

Kutokana na mmomomyoko wa maadili uliopo kwa sasa, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kunusuru kikazi cha sasa na kijacho.

Hofu ya Mungu, upendo na kudumisha undugu vimepungua sana badala yake ukatili, chuki, visasi vimechukua nafasi kubwa. Hapa kuna tatizo kubwa.

Vyombo vya habari; runinga, magazeti na redio kila uchwapo vimekuwa vikitoa taarifa za uhalifu huu na ule katika maeneo mbalimbali ya nchini yetu.

Uhalifu huu umekuwa ukisababisha vifo vya watu, matatizo ya kisailojia ya kudumu, ulemavu au kukosa mali, hali inayorudisha nyuma maendeleo ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Kujenga maadili mema ya mtu kunagusa wadau wengi, lakini msingi mkuu unaanzia katika familia.

Ninapenda kwa dhati kabisa kumpa kongole mwimbaji wa nyimbo za Injili, Daniel Thomas aliyetunga wimbo uitwao "Ibada Njema" ambapo katika wimbo huo alisisitiza kuwa mambo mazuri kwa mtoto yanajengwa kuanzia nyumbani, yaani katika familia.

Mwimbaji Daniel katika wimbo huo alisisitiza kujenga kwanza mambo ya nyumbani kabla ya kujenga sehemu nyingine. Kwamba kushindwa kujenga maadili bora katika ngazi ya familia ndipo kunapoleta ugumu kwa walimu mashuleni, viongozi wa dini kwa waumini wao na viongozi wa serikali kwa watumishi na wananchi wanao waongoza.

Mtoto anapokosa msingi bora wa malezi yaliyojaa maadili mema katika ngazi ya familia, kumrekebisha kwingineko inawezekana lakini kunakuwa na ugumu kwelikweli. Ndio maana wahenga wakasema "samaki mkunje angalia mbichi". Kwamba ukijaribu kumkunja wakati ameshakauka hakunjiki abadani, badala yake anakatika vipandevipande!

Hata maneno ya Mungu katika Mithali 22:6, Biblia inasema "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee".

Mstari huu unaweka kielelezo cha kujenga tabia na maadili mazuri kwa watoto katika ngazi ya familia ambapo wazazi na walezi wanawajibika moja kwa moja kufanya jukumu hili.

Wanasaikolojia wanaamini kila mtu anazaliwa akiwa na tabia njema, hivyo anahitaji mwendelezo wa kulelewa katika malezi na maadili mazuri ili kuendelea kuwa na tabia na maadili mazuri.

Waarabu wana msemo kwamba 'Al-ummu madrasa', wakimaanisha kuwa mama ni shule, ana wajibu mkubwa wa kumfanya mtu unayemwona mbele yako wakati unaposoma makala hii, awe kama alivyo; muungwana au mtu wa hovyo!

Ninachojaribu kusema hapa ni kwamba ugumu uliopo wa kujenga tabia na maadili bora unaweza kupungua au kumalizika kabisa kama wazazi na walezi watatimiza kikamilifu jukumu la kulea watoto wao katika maadili yanayokubalika na jamii. Katika vitabu vyote vya dini, Mungu anawaagiza wazazi na walezi kuwafundisha watoto tabia na madili mazuri.

Katika Dini ya Kiislamu, kwa mfano, mafundisho yanaonesha wapo wazazi ambao siku ya Kiama watakuwa na thawabu za kuwawezesha kwenda peponi lakini watoto wao watapiga kelele mbele ya Mungu kwamba hawakuwakanya kuacha maovu na hivyo watashangaa kuona madhambi ya watoto wao yanakula thawabu zao na kujikuta wanaingia motoni.

Moja ya kozi niliyojifunza wakati nasoma Shahada ya Uzamili ya Sanaa katika Elimu ya Kikristo (Master of Arts in Christian Education) katika Chuo Kikuu cha Kikristo cha Elam (Elam Christian University) ni kozi ya "Utangulizi wa Elimu ya Kikristo – Introduction to Christian Education".

Katika kozi hiyo, nilijifunza historia ya maendeleo ya elimu ya dini wakati wa Agano la Kale, ambapo wazazi wa Kiyahudi walipewa jukumu la kuwafundisha watoto wao na watoto wa watoto wao (wajukuu) kuhusiana na elimu ya dini.

Pia, nyumbani kukawa sehemu muhimu ya mafunzo kwa watoto (The home became the most important place for instruction of children). Mstari wa kusimamia ulikuwa katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati 6:6-9, Biblia inasema "Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako".

Maagizo haya yalikuwa nyenzo muhimu ya kusaidia kujenga jamii yenye maadili mazuri ambayo ni jambo zuri hata mbele za Mwenyezi Mungu.

Ukatili, ubakaji, mauaji ya kutisha, wizi na ujambazi ni matokeo ya mmomonyoko wa maadili. Kama watoto watafundishwa maadili mema katika hatua za mwanzo kabisa za ukuaji wao, yaani kufundishwa nyumbani na wazazi au walezi wao kuna uwezekano mkubwa wa kujenga jamii yenye maadili mazuri.

Mtoto anayefundishwa huku akikemewa kujua kwamba kusema uongo ni kosa, kutoheshimu mwingine ni kosa, upendo kwa wengine ni lazima, ni muhimu kuheshimu mali ya mwingine, kusengenya ni kosa na mengine mfano wa hayo si rahisi kufanya matendo hatari kama ukatili, wizi na mauaji.

Vijana wanaojulikana kama 'Panyarodi' ambao wamekuwa wakifanya vitendo mbalimbali vya uhalifu yakiwemo mauaji ya watu wasio na hatia hawatakuwepo ikiwa watoto watalelewa katika maadili mazuri ya Kumcha Mungu huku juhudi hizo zikianzia katika ngazi ya familia.

Ibada njema ya kuwafundisha watoto na vijana maadili na tabia njema ianzie nyumbani kwanza, ndipo baadaye iendelee katika nyumba za ibada, shuleni na sehemu nyingine.

Gharama za kujenga maadili mazuri kabla mambo hayajaharibika ni ndogo kuliko gharama za kujenga maadili baada ya mmomonyoko wa maadili kutokea.

Ukiona inafikia mahala mtoto hamsikilizi mzazi wake, mtoto hamjali mzazi wake huku wengine wakifikia kuwatukana au kuwapiga kabisa wazazi wao, basi ujue wazazi haohao wanavuna walichopanda. Huo ndio ukweli mchungu!

Jamii tubadilike ili kujenga jamii yenye upendo, amani, utulivu na maendeleo kwa sababu tukifeli kujenga maadili na malezi mema nyumbani, tumefeli pakubwa mno. Tusifikie kwenye msemo wa Kiswahili wa 'asiyefunzwa na mama, hufunzwa na ulimwengu'. Kwa nini mtoto afunzwe na ulimwengu?

Ndiyo maana nasema, ibada njema ya kujenga maadili mena kwa mtoto, kama alivyoimba Daniel, inaanzia nyumbani na sio shuleni, ofisini, kanisani wala msikitini.



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Misumari ya mahusiano - 3

WIKI iliyopita tuliendelea na somo hili lenye makusudi ya kuimarisha mahusiano yetu. Mambo haya unaweza kuyachukulia kirahisi au 'poa' kama wanavyosema vijana wa siku hizi na hivyo kutoyapa uzito unaostahili lakini ukiyazingatia na kuamua kwa dhati kuyatekeleza, huleta uimara wa mahusiano.

Mbali na uimara huleta pia amani na kuwajengea furaha walio katika mahusiano. Karibu tuendelee na safu hii sehemu ya tatu kwa faida yako na ustawi wa jamii yetu.

### 11. KUJALI (EMPATHY)

Kujali ni jambo la msingi. Kuoneshana moyo wa huruma na kujali kwenye mahusiano kumepotea sana katika zama tulizonazo. Jambo hili hata si gharama, ni kuonesha kwamba unamhurumia mwenzio, unajua hali anayoipitia na kwamba hali anayoipitia nawe inakugusa na ikiwezekana kuonesha kumsaidia au kushiriki naye hali anayoipitia iwe furaha au huzuni.

Pamoja na kuwa jambo hili ni muhimu pande zote, ni muhimu zaidi kwa mwanamke. Hili kwa mwanamke ni hitaji la msingi sababu ni moja. Kwamba kati ya msingi unaojenga au kuibua hisia, na sote tunatambua kuwa mwanamke anaishi vyema katikati ya hisia. Mfano, kuwa mwanamke tu, ni changamoto ya kutosha.

Mwanamke anakabiliana na hedhi kila mwezi, ujauzito, kunyonyesha watoto, watoto wachanga wanaolia kwa mihemko, vijana wenye maamuzi magumu na hatimaye, kuingia kwenye umri wa ukomo wa hedhi. Yote haya yanaendelea wakiwa wanashughulika na ndoa, kazi, maisha ya familia, na mengine mengi.

Ni katika muktadha huo, wanawake wanataka mwanaume anayegundua yote wanayofanya na kuonesha japo kujali kidogo. Wanahitaji mwanaume awasaidie kupunguza mzigo, kuuliza jinsi wanavyojisikia, kumpigapiga bega na kumwambia "pole, natambua umechoka", na kwa ujumla kuonesha msaada fulani.

### 12. URAFIKI (FRIENDSHIP

Kwenye mahusiano kunahitaji urafiki. Urafiki unahusisha kuamianiana na kutegemeana. Urafiki unahitaji kila mtu kuwa mwelewa. Marafiki hawagombanigombani sababu ya mwenza kufanya makosa kwa kuwa wanaelewana na wanachukuliana.

Urafiki unahitaji mipaka. Kinachowatatiza watu kwenye mahusiano na kuondoa urafiki ni kutaka kutumia zaidi dhana ya kumilikiana (ownership) badala ya dhana ya urafiki na ushirika kwa maana ya (partnership).

Kwa sababu ya dhana ya anataka ajue kila kitu kuhusu mwenzi wake, ambadilishe kila kitu mwenzi wake awe anavyotaka yeye na anataka maisha ya amri yatawale. Mambo haya huutupa nje urafiki na matokeo yake ladha ya mahusiano hupotea.

Mfano mwanaume anataka mke awe rafiki yake. Anataka kutumia muda pamoja naye na kupumzika tu. Anataka kuangalia mechi za mpira au kucheza mchezo wa video bila kusumbuliwa mara kwa mara na kumbusho la bili, kuombwa hela na majukumu (hayo yawe na wakati wake na yawe na mantiki).

Mwanaumke anataka mkiwa wote awe huru kupokea simu zake na kujibu jumbe za watu wake. Pia anataka kuwe na nyakati za kupeana tahadhari na kukumbushana mambo ya msingi. Vilevile anataka aweze kuachilia na kukufungulia moyo wake bila kuchunguzwachunguzwa na kulaumiwa.

Vivyo hivyo mwanamke anahitaji kupendwa, anahitaji kuelimishwa kwa upendo na siyo ukali kila mara na kufokewa.

Tatizo ambalo mara nyingi linaambatana na urafiki ni pale ambapo mtu anaoneshwa urafiki halafu yeye anaonesha hali ya kuchukuliana poa na kumwona mwenzi kawaida. Tahadhari ni kuwa mnapooneshana urafiki, kila mmoja asisahau wajibu wa msingi kwa mwenzi wake. Mwanaume ana wajibu wa kupenda kwa dhati na mwanamke anahitaji kutii kwa kila jambo. Ili urafiki udumu, kimaumbile, wanaume wanapenda furaha na heshima.

> "Mwanaumke anataka mkiwa wote awe huru kupokea simu zake na kujibu jumbe za watu wake. Pia anataka kuwe na nyakati za kupeana tahadhari na kukumbushana mambo ya msingi. Vilevile anataka aweze kuachilia na kukufungulia moyo wake bila kuchunguzwa chunguzwa na kulaumiwa.

### 13. MOYO WA SHUKRANI (BEING GRATEFUL)

Pande zote za mahusiano zinahitaji moyo wa shukrani. Ni vizuri ieleweke, hapa naongelea moyo wa shukrani. Hii ni kinyume cha manung'uniko, lawama na huzuni.

Kwa mfano, kama ilivyo kwa wanawake, wanaume kwao ni zaidi, hupenda wenzi wanaoshukuru. Ni kama Mungu tu, anachukia manung'uniko.

Wakati mwenzi wako anajitahidi kufanya jambo zuri kwako, mwoneshe jinsi unavyoshukuru. Hii ioneshwe kwa fikra zako na kwa unyenyekevu wako. Jambo hili litasaidia sana kumtia moyo na kumpa kujiamini. Thamini juhudi zake za kukufurahisha au kuwa mwenzi bora, hata kama ni kidogo. Niamini mimi, atafurahi, atahamasika na kufanya zaidi.

### 14. UKARIMU (GENEROUSITY)

Hakuna mtu anayetaka mwenza mchoyo. Lazima uwe mkarimu kwa pesa yako, mali zako, hisia zako (mtazamo), muda wako, mwili wako, nk . Hakuna kitu ndani ya uwezo wako kinachopaswa kuwa kingi kumpa mwenzi wako kama ukarimu.

Pamoja na kuwa hili ni hitaji la pande zote, mwanaume unashauriwa kuwa mkarimu zaidi. Wanawake hawachoki kamwe, wanapenda kufanyiwa matendo ya ukarimu, kununuliwa na waop kununua vitu, kupendeza, kupiga picha, nk. Hivyo mwanaume tambua hilo na mara kwa mara kadri unavyoweza kumudu, jitahidi kutimiza hayo kwa sababu mwanamke anastahili.

**Wework Consult - Your Partner in Growth.**

**Itaendelea wiki ijayo...**





**Na Hamisi Kibari**

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 16

**Chris, mwanaume ambaye biashara yake ya kuuza mbao na vifaa vya ujenzi ilikuwa inakwenda vyema ghafla inachungulia kaburi. Haya yote ni tangu alipokutana na mrembo aliyekuwa akitikisa mji wa Tabora, Joyce na kuanzisha uhusiano naye. Mapenzi yao yanakuwa chanzo cha kumpinga mkewe hadi kupoteza fahamu na baadaye daktari kumjulisha kwamba mkewe amefariki dunia. Chris anachukua ushauri wa daktari kuficha kifo cha mkewe, hali inayofanya atumie gharama kubwa. Baada ya kufilisika, Joyce anamkataa Chris na kugeukia kwa mwanaume mwingine na kusababisha Chris afanye fujo kubwa ya kumpinga Joyce na huyo mpenzi wake mpya na kuanza kutafautwa na polisi. Kutooneka kwake kunaleta wasiwasi mwingine hadi dada yake kufikiria kutoa picha kwenye magazeti. Lakini kuna simu yenye taarifa kuhusu Mama Kenny... Ni zipi hizo? Endelea.**

"Naitwa Maua, maarufu Mama Jane. Ninaishi Mihogoni, hapa jirani tu na alipokuwa akiishi Mama Kenny na mumewe."

"Tunafahamiana?"

"Mimi ninakufahamu lakini nadhani wewe hunifahamu."

"Unasemaje Maua."

"Nilikuwa nina habari zinazomhusu wifi yako, Mama Kenny…"

"Habari za Mama Kenny? Zilikuwa zinasemaje dear?" Alimkata kauli.

"Ni habari ndefu…"

"Nina hamu sana kuzisikia. Enhe! Zinasemaje?"

"Nilikuja leo shuleni ili tuzungumze lakini nimekuta umeshaondoka. Nimeambiwa leo umeondoka mapema ndio nikapata namba yako ya simu."

Maneno yake yalimshitua Mwalimu Misango. Akahisi mapigo ya moyo yanabadilika.

"Aisee, habari za Mama Kenny kama unazo nina hamu sana kuzisikia. Nzuri mbaya?"

"Mchanganyiko?"

Jibu hilo lilizidi kumchanganya Mwalimu Misango.

"Enhe, nimegee kidogo."

"Hizi si habari za kuzungumzia kwenye simu. Kama unaweza njoo hapa nyumbani."

"Nitakuja baadaye nikitoka hospitali. Sasa hivi ninajiandaa kwenda kumwona daktari na ndio maana leo nimeondoka shuleni mapema."

"Pole Mwalimu, unaumwa?"

"Hapana, ni mtoto wa huyo jirani yenu?"

"Kenny anaumwa?"

"Hapana. Ni huyu mdogo, Huba."

"Poleni sana."

"Ninataka nimpeleke hapo Hospitali ya Huruma. Huwezi kuchukua bodaboda ukaja tukazungumzia hapohapo hospitalini? Nitalipa."

"Mh! Nitaangalia…"

"Tafadhali njoo. Mbali na kulipia usafiri wa bodaboda kuja na kurudi, nadhani ni hazizidi Sh 2,000 kwa kila safari, lakini pia nitakupa Sh 10,000 ya usumbufu. Yaani nina hamu sana ya kusikia habari za wifi yangu Mama Kenny lakini nadhani tatizo la hali ya mtoto linapaswa kushughulikiwa kwanza ndio maana ninashindwa kuja huko kwako kwanza," alisema Mwalimu Misango.

"Basi Mwalimu, baada ya saa moja na nusu hivi nitakuwa ninaondoka kuja hapo Huruma Hospital. Nadhani utakuwa umeshaonana na daktari na kupata majibu ya vipimo muda huo… Wakati unaingia kwa daktari, utanipigia simu."

"Ukiwahi kidogo itakuwa vyema. Labda baada ya dakika 40. Tutapata muda wa kuongea hata wakati nitakapokuwa kwenye foleni ya kumwona daktari. Mara ya mwisho kwenda hapo Huruma sikuona watu wengi."

"Lakini kama utachukua na vipimo, haiwezi kuwa chini ya saa moja."

"Basi wakati ninarudisha majibu kwa daktari nitakupigia."

"Sawa."

***

Mwalimu Misango aliketi kwenye benchi la kuingia kwa daktari akiwa amempakata Huba na kumpigia simu Maua lakini simu haikupokelewa.

Kwa kuwa ilikuwa imepita saa moja na dakika kadhaa tangu azungumze naye akahisi kwamba huenda alikuwa kwenye bodaboda ndio maana hapokei simu. Hata hivyo, akamtumia ujumbe mfupi wa maandishi kwamba ndio kwanza alikuwa akijiandaa kuingia kwa daktari na kwamba hakukuwa na watu wengi chumbani kwa daktari wa watoto jioni hiyo.

Aliendelea kukaa akiangaza macho huku na kule akitegemea kumwona Maua lakini hakumwona. Mtu aliyekuwa mbele yake alipoingia kwa daktari akajaribu tena kumpigia simu lakini kama mwanzo haikupokelewa. Hadi anaingia kwa daktari, Maua alikuwa hajatokea wala kujibu simu yake.

"Imekuwaje tena huyu Maua," akajisema wakati akiingia kwa daktari.

Muda mfupi wakati akiwa kwa daktari, akaona ujumbe mfupi wa maandishi ukionesha kwamba Maua alikuwa ameshafika hospitalini hapo na hivyo alikuwa akimsubiri nje.

**Basi Mwalimu, baada ya saa moja na nusu hivi nitakuwa ninaondoka kuja hapo Huruma Hospital. Nadhani utakuwa umeshaonana na daktari na kupata majibu ya vipimo muda huo... Wakati unaingia kwa daktari, utanipigia simu.**

Ujumbe ule ulimpa kiwewe. Kimsingi kadri muda ulivyokuwa unasonga mbele ndivo alivyokuwa akipata hamu ya kumwona Maua ili kumpa habari za Mama Kenny.

Majibu yalionesha kwamba Huba alikuwa akisumbuliwa na malaria tu na si UTI kama alivyohisi Mwalimu Misango awali, hivyo daktari akamwandikia dawa na kumsisitiza kuhakikisha mtoto huyo analala kwenye chandarua.

Kama alivyotarajia, alipotoka kwa daktari alimkuta Maua ambaye alikuwa amevaa baibui na ushungi akimsubiri nje.

Kwake ilikuwa ni sura mpya. Alijitahidi kumwangalia kwa sababu mwanamke huyo wa Kiislamu licha ya kujitanda ushungi lakini alikuwa ameacha sura yake wazi na bado hakumfahamu. Ilikuwa kama ni mara ya kwanza kumwona.

Kwa jinsi alivyokuwa na hamu ya kusikia habari za Mama Kenny huku akitaka asimcheleweshe Maua, akaona wazungumze kwanza ndipo baadaye akachukue majibu.

Japo ilionekana kwamba Huba alikuwa na malaria lakini jioni hiyo alikuwa akicheza, bila shaka ni kutokana na dawa za kuondoa maumivu alizokuwa amempa.

"Niambie Maua, yaani nina hamu sana ya kusikia habari za Mama Kenny. Huu umeingia mwezi wa 10 habari zake hazifahamiki. Ndugu zake wa damu naona kama wamekata tamaa kumtafuta. Kinacholeta mashaka makubwa ni kwa nini, kama yuko hai atelekeze watoto wake? Siamini kama kuna mama wa aina hiyo. Kama wapo ni wachache. Mwanzoni nilijua kaamua kulipiza kisasi baada ya mumewe kumletea mwanamke nyumbani kwa sabanu aliwahi kuniambia kwamba anaweza akamua na yeye kutafuta bwana akidai wako wengi wanaomtaka lakini hiki kimya chake cha muda mrefu si cha kawaida," alisema Mwalimu Misango.

"Hilo ndilo limenileta kukueleza ukweli na mkanganyiko ambao umejitokeza kwenye mtaa wetu."

"Nieleze Maua kile unachokijua."

"Kimsingi, sisi pale mtaani tunajua kwamba siku moja usiku, Baba Kenny alimpiga sana mkewe. Yaani alikuwa anapiga kelele kwamba 'unaniua unaniua'. Majirani kadhaa wakiwemo mume wangu walitoka na zile kelele zikazimika ghafla. Watu wanahisi kwamba mdogo wake alimuua mkewe na pengine alikwenda kumtupa anakopajua yeye."

"Duh! Una hakika na maneno yako?"

"Asilimia 100. Kila mtu pale mtaani anajua kwamba Mama Kenny aliuawa kwa kipigo na baada ya Baba Kenny kumuua, akatoka akiwa na huyo hawaraka yake, yule msichana aliyewahi kuwa Miss Tabora. Watu wanaamini alirudi baadaye na kwenda kuzika au kutupa mwili wake."

"Kama ni kweli, unadhani kwa nini watu wamekuwa kimya kiasi hiki. Mwezi wa 10 sasa watu wanajua Mama Kenny aliuawa halafu wamekaa kimya!"

"Wanaogopa kutoa ushahidi. Imebaki minong'ono tu mtaani lakini mimi nimeona ni vyema hili likawa wazi. Na hasa kilichonifanya nikutafute ni watu kuanza kuona mauzauza ya Mama Kenny pale mtaani."

"Mauzauza?"

"Ndiyo… Mzimu wa Mama Kenny umekuwa ukija mtaani kwetu. Jana ilikuwa mara ya pili kama si ya tatu."

"Mzimu wa Mama Kenny?"

"Ndiyo. Na hii safari ya pili mimi mwenyewe nimeshuhudia. "

"Kivipi?"

"Mtu kama Mama Kenny ameshaonekana pale mtaani mara mbili. Unakuja akiwa katika gari aina ya IST nyeusi. Bila shaka sisi tunaona ni gari lakini pengine hicho ni kitu kingine."

"Bado sikuelewi Maua!"

"Siku ya kwanza, watu waliona gari ikisimama kwenye nyumba ya Baba Kenny ambayo imeuzwa. Ilikuwa ni wiki moja baada ya aliyeinunua kuanza kuikarabati. Kama hujaiona tangu imeanza kukarabatiwa leo ukioona Mwalimu utaipotea kwa jinsi ilivyopendeza. Watu waliona gari ikisimama upande wa pili wa barabara kisha akashuka mwanamke aliyekuwa amejitanda ushungi. Waliomwona wanasema alisimama akiiangalia ile nyumba akiwa ameegemea gari. Mwanangu aliyekuwa anapita kuja ndani, ni mmoja wa waliomwona. Mwanzo hakufikiria kama anaweza kuwa Mama Kenny kutokana na mavazi. Mtaani hatujawahi kumwona Mama Kenny akiwa amejitanda ushungi, amevaa kama Muislamu anayetaka kuingia msikitini kuswali. Yaani alivaa kama mimi nilivyo.

"Sasa walipokutanisha macho akagundua ni Mama Kenny. Akamsalimia, akaitikia kwa kubabaika na mara akageuka na kuingia kwenye gari harakaharaka na kuondoka kwa kasi," alisema Maua huku Mwalimu Misango akiwa amemtumbulia macho.

*ITAENDELEA*

# Mtanzania aliyetaka kutatua mzozo wa mateka wa Marekani nchini Iran

**Na BBC**

MZOZO wa utekwaji nyara wa raia wa Marekani nchini Iran, ulioanza Novemba 4, mwaka 1979, ulikuwa ni moja ya matukio makubwa na muhimu yaliyotokea wakati wa uongozi wa Rais Jimmy Carter, nchini Marekani.

Mgogoro huo uliodumu siku 444 ulihusisha mateka 52 raia wa Marekani na mamia ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Iran, ambao waliuteka ubalozi wa nchi hiyo mjini Tehran.

Tukio hilo lilibadilisha kabisa mwelekeo na uhusiano kati ya Marekani na Iran wakati tayari kukiwa na mazingira ya wasiwasi ya wakati wa vita baridi.

Kwa sababu kadhaa, mzozo huo pia ulichangia kwa hakika kwa Rais Carter kusalia madarakani kwa muhula mmoja na kushindwa uchaguzi dhidi ya Ronald Reagan.

Suala hilo la uchaguzi pamoja na mipango ya Marekani ya majaribio ya kuwaokoa mateka, yanajulikana na umma.

Kile ambacho hakijulikani ni kuwa mwanzoni mwa mgogoro huu, Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambaye alikuwa mwanadiplomasia wa Tanzania aliyekuwa na umri wa miaka 37, alifikiriwa kuwa msuluhishi ambaye angeweza kusaidia kuachiliwa mateka hao na kufanya mapatano na Ayatollah Khomeini mjini Tehran.

Mwanadiplomasia huyo alikuwa Salim Ahmed Salim, Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa.

Ingawa safari ya Tehran haikuwahi kutokea, hasa kutokana na siasa na kuzuiwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa wakati huo Kurt Waldheim aliyekuwa anataka kuchaguliwa tena mwaka 1981.

Imani aliyopewa na kujiamini kwake Salim kuwa ana uwezo wa kushiriki na kuipatanisha Iran na Marekani, vilitoa nafasi ambayo haijawahi kushuhudiwa kuhusu jinsi wanadiplomasia wa Kiafrika wanavyoweza kuwa na ushawishi katika korido za Umoja wa Mataifa.

Pia inaonyesha jinsi Tanzani na wanadiplomasia wake walivyoheshimika katika kipindi ambacho mataifa yenye nguvu duniani yalivyokuwa yanaifinyanga dunia na mataifa mengine, hasa ya Afrika, yalivyokuwa watazamaji tu.

Matokeo ya mustakabali wa Balozi Salim kugombea nafasi ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwaka 1981 na juhudi za kuchaguliwa tena za Rais Carter, yalikuwa matukio mawili yaliyoathiriwa kwa kushindwa kupatikana kwa utatuzi wa haraka wa mzozo wa mateka jijini Tehran.

Kwa mujibu wa maelezo binafsi ya Dk. Salim na Balozi wa Marekani wa wakati huo, iwapo Carter angeshinda tena uchaguzi, yeye (Dk. Salim) angekuwa na nafasi kubwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa UN. Ikiwa Reagan angeshinda, 'mambo yangebadilika kabisa.'

Balozi wa Marekani alikuwa sahihi. Rais Carter alishindwa katika uchaguzi mkuu 1980 na Ronald Reagan. Dk. Salim naye alishindwa kupata kura za kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakati wa uchaguzi wa 1981.

Marekani ilipiga kura ya turufu dhidi ya Dk. Salim kila mara katika duru 16 za upigaji kura katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Mjadala hasa, sio kile ambacho kingeweza kutokea. Habari kuu hasa ni kuwa bila maelezo ya kina na uwekaji kumbukumbu wa Dk. Salim, tusingeweza kamwe kujua kuhusu uwezekano wa kwenda Tehran na jukumu la diplomasia ya Tanzania katika kupunguza mvutano na kutafuta suluhu ya moja ya migogoro mikubwa iliotokea 1979.

Kutokuwepo kwa kumbukumbu hizi ingekuwa ni hasara kwa wale wanaothamini historia na wana shauku ya kuelewa jinsi wanadiplomasia wa Tanzania walivyokuwa na ushawishi katika nyanja za kimataifa.

**Mjadala hasa, sio kile ambacho kingeweza kutokea. Habari kuu hasa ni kuwa bila maelezo ya kina na uwekaji kumbukumbu wa Dk. Salim, tusingeweza kamwe kujua kuhusu uwezekano wa kwenda Tehran na jukumu la diplomasia ya Tanzania katika kupunguza mvutano na kutafuta suluhu ya moja ya migogoro mikubwa iliotokea 1979.**



Rais wa zamani wa Marekani Jimmy Carter.

Kwa kila kipande kisichoelezwa cha historia, tunapoteza sehemu yetu wenyewe.

Na hiyo ni moja ya sababu kuu ya kuanzishwa Tovuti ya Kumbukumbu ya Salim Ahmed Salim.

Tulitaka kuhakikisha matukio yaliyorekodiwa yanapatikana kwa urahisi kwa lengo la kuhifadhi sehemu ya historia yetu.

Ulianza kama mpango unaoendeshwa na familia, tovuti ya kumbukumbu hizi ni mradi wa kitaifa na wa Kiafrika na fursa ya kusimulia kipekee habari za Afrika kuhusu siasa za kimataifa kwa mtazamo wetu.

Tumezoea kuona mawasiliano kutoka kwa viongozi wa kigeni kwenda kwa wakuu wa nchi au serikali za Kiafrika, lakini ni marachache mno kuona majibu.

Tumezizoea hizi siri, ikiwa ni pamoja na matukio yetu ya kihistoria, kufichuliwa na watu wengine – mtazamo huu unapaswa kubadilika na kukumbatia historia zetu. Kufahamu mambo yaliyojiri katika vyumba na korido zilizounda historia, ni muhimu kwa Waafrika na vizazi vijavyo.

Matumaini yetu ni kwamba Tovuti ya Kumbukumbu ya Salim Ahmed Salim itawahimiza viongozi na serikali za Afrika kueleza zaidi habari ya yale yaliyojiri huko nyuma, ili kuonyesha jukumu la Afrika katika kuunda siasa za kimataifa.

Kwa kufanya hivyo, wanadiplomasia wa Afrika wataweza kuunda na kushawishi mustakbali wa usoni - ambapo inakadiriwa asilimia 25 ya idadi ya watu ulimwenguni itakuwa ni kutoka bara hili ifikapo 2050.



Dk. Salim Ahmed Salim.

# Jose Mourinho ni Kocha mfanyabiashara mjanjamjanja

## ■ Anavuna mamilioni kwa kufukuzwa kazi




**Na Valensi Mbaga**

JOSE Mourinho bila shaka ni mmoja wa makocha wakubwa wa wakati wote na pia ndiye mtu hatari wa mazungumzo ya malipo makubwa anapofukuzwa.

Katika maisha yake mashuhuri ya usimamizi, Mourinho amesimamia zaidi ya mechi 1000 za kandanda na kushinda mataji 26 kwa wakati huo yakiwemo mataji manane ya ligi na mawili ya UEFA Champions League.

Meneja huyo wa Ureno ataingia kwenye historia kama meneja bora wa muda wote lakini mara nyingi hadumu na klabu moja kwa muda mrefu sana

Siku za karibuni alipoteza kibarua chake katika klabu ya Roma, kufuatia mwendo usiobadilika ambao ulifanya kikosi cha Mourinho kikishinda mechi moja kati ya sita zilizopita.

Zifuatazo ni takwimu za malipo ya Jose Mourinho katika kila timu alizofundisha na kuvunjiwa mkataba.

**Chelsea (2007)**

Mara ya kwanza Mourinho akiwa Chelsea alikuwa na kila kitu. Akitazamwa wakati huo kama meneja mpya kuleta mafanikio zaidi, Mourinho alithibitisha haraka kwamba uvumi aliokuja nao ulikuwa wa msingi.

Chelsea ilishinda mataji mfululizo ya ligi chini ya aliyejitangaza kuwa Special One huku akiibeba Uingereza kwa dhoruba. Mourinho kisha bila kutarajia aliondoka Chelsea katika msimu wake wa tatu na klabu hiyo kufuatia kuanza kwa msimu polepole.

Baada ya kuondoka klabuni hapo, meneja huyo alikubali kulipwa fidia ya takriban pauni milioni 18 kufuatia mechi 185 akiwa kocha.

**Real Madrid (2012)**

Baada ya Mourinho kufanikiwa kushinda mataji matatu matatu akiwa na Inter Milan msimu wa 2009-10, mvuto wa Real Madrid ulikuwa mkubwa sana kwa Mourinho kukataa.

Mourinho anaweza kuwa ameshinda mataji matatu pekee wakati wa kukaa kwake kwa miaka mitatu huko Madrid, lakini hiyo ilitokana na ukweli kwamba alikuwa akipambana na timu kubwa zaidi ya Barcelona wakati wote.

Timu yake ya Real Madrid iliweka rekodi iliposhinda taji la ligi ya 2011-12 na kuwa timu ya kwanza kabisa kuvunja pointi 100 kwenye La Liga huku pia ikivunja rekodi ya ufungaji wa muda wote kwa mabao 121.

Mourinho aliondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu wake wa tatu huku timu yake ikimaliza nafasi ya pili kwenye La Liga na kutoka katika Ligi ya Mabingwa

>>Inaendelea uk. 21

# Jose Mourinho ni Kocha mfanyabiashara mjanjamjanja

>>Inatoka uk. 20

katika nusu fainali. Alipokea kitita cha pauni milioni 17 kama sehemu ya kifurushi chake cha fidia.

**Chelsea (2015)**

Nafasi ya pili ya Mourinho huko Stamford Bridge ilikuwa ya machafuko sawa na ya kwanza. Alishinda Ligi ya Premia katika msimu wake wa pili akiwa na timu kabla ya mambo kumuendea sawa tena katika mwaka wake wa tatu.

Huku Chelsea wakiwa katika nafasi ya 16 kwenye jedwali mwezi Disemba walichukua uamuzi wa kuachana na Mourinho kwa mara ya pili. Safari hii walilipa kitita cha pauni milioni 12.5 ili kumuondoa.

**Manchester United (2019)**

Kila mtu alimcheka Mourinho alipodai kumaliza nafasi ya pili akiwa na Man United ni moja ya mafanikio yake makubwa zaidi kuwahi kuyapata, lakini ilibainika kuwa alikuwa anafanya jambo fulani.

Muda wake Old Trafford haukuwa wa kuvutia kuliko kazi zake za awali, lakini alifanikiwa kushinda mataji matatu katika msimu wake wa kwanza akiwa na klabu hiyo.

Kwa mtindo wa kawaida wa Mourinho, timu iliamua sasa kutosha wakati wa msimu wake wa tatu na kuamua kumpa mkono wa kwaheri. United walilipa takriban pauni milioni 15 kumng'oa mnamo Desemba 2019.

**Spurs (2021)**

Kuwasili kwa Mourinho huko Spurs mnamo 2019 kulikuja kama mshtuko kwetu sote, cha kushangaza zaidi ni ukweli kwamba walimfukuza kabla ya fainali ya Kombe la EFL.

Meneja huyo wa Ureno aliiongoza Spurs mechi 86 kabla ya kutimuliwa Aprili 2021 na malipo yake ya fidia yalifikia pauni milioni 16.

**Roma (2023)**

Mourinho kisha alifanikiwa kuiongoza Roma kumaliza mechi za Ulaya mfululizo katika miaka yake miwili ya kwanza akiwa na klabu hiyo. Pia alijishindia fedha kwa kushinda UEFA Europa Conference League.

Walakini, mambo yalianza kwenda mrama katika msimu wake wa tatu na timu ya Italia ilifanya uamuzi wa kuachana na mzee huyo wa miaka 60.

Mourinho aliripotiwa kupokea mshahara wa kila mwaka wa takriban Euro milioni 9 huko Roma na mkataba wake ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu.

Kwa jumla, Mourinho ameingiza kiasi cha pauni milioni 84 katika kipindi chote cha kazi yake ya ukocha kupitia klabu zinazomuondoa. Na kwa pande wake kuwa na faida zaidi






# Siyo Salah wala Mane

IVORY Coast

KINARA wa magoli kwenye michuano ya Kombe la Mataifa Afrika AFCON 2023 siyo Mo Salah, Victor Osimhen, Sadio Mane, Inaki Williams wala Nicolas Jackson.

Emilio Nsue wa Guinea ya Ikweta ambaye kiasilia anachezea nafasi ya beki wa kulia katika klabu ya CF Intercity ya Ligi daraja la tatu Uhispania ndio kinara wa magoli AFCON 2023 akiwa na magoli matano.

Nsue ambaye pia anamudu kucheza kama winga wa kulia amefunga magoli matano kwenye AFCON 2023 yakiwemo hat-trick dhidi ya Guinea Bissau na magoli mawili leo dhidi ya wenyeji, Ivory Coast.

Laurent Pokou ndio mchezaji pekee aliyewahi kufunga magoli mengi zaidi (7) kwenye hatua ya makundi ya michuano ya AFCON kumzidi Nsue mwenye mwenye matano.

### MSIMAMO WA WAGUNGAJI AFCON 2023

Emilio Nsue —5
Baghdad Bounedjah—3
Lamine Camara—2
Mohammed Kudus—2
Bertrand Traore—2
Themba Zwane— 2
Mostafa Mohamed—2



# Huyu Emilio Nsue ana balaa

IVORY Coast

NSUE Emilio alishinda Euro 2007 U-19 na Euro 2011 U-21 akiwa na Timu ya Taifa ya Uhispania, akicheza pamoja na Dani Parejo, Thiago, Juan Mata, David de Gea na wengineo.

Akiwa na umri wa miaka 34, Emilio Nsue ndiye anayeongoza kwa ufungaji bora wa Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023( akiwa na mabao matano.


Kwenye Mechi ya pili ya Makundi dhidi ya Guinea-Bissau, alikua mchezaji mzee zaidi kukamilisha hat-trick katika historia ya mashindano hayo.

Katika mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi, Nsue amefunga mabao mawili katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Côte d'Ivoire, na kuwaondoa wenyeji kwenye mashindano.

Kwa mara ya kwanza katika historia yao, Equatorial Guinea wamemaliza wakiwa juu ya kundi lao na nahodha wao amekuwa na jukumu kubwa la kuhakikisha hivyo.







# CAF yachunguza vurugu za Congo na Morocco

IVORY COAST

SHIRIKISHO la Soka Barani Afrika (CAF) limeanza kufanya uchunguzi juu ya ugomvi uliotokea kati ya Kocha Mkuu wa Morocco ,Walid Regragui dhidi ya Mshambuliaji wa DR Congo ,Chancel Mbemba kwenye mechi iliyoisha kwa sare ya 1-1 kati ya DR Congo dhidi ya Morocco wiki iliyopita

# Ivory Coast yaweka rekodi

IVORY COAST

BAADA ya kuondolewa hii leo kwenye Michuano ya AFCON 2023,Ivory Coast imeweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza mwenyeji kupoteza michezo miwili ya hatua ya makundi ya AFCON tangu mwaka 1984.

Timu ya mwisho kufanya hivyo pia ilikuwa ni Timu ya Taifa ya Ivory Coast



# Mabingwa wa AFCON tangu 1957

Mwaka 1957: Egypt
Fainali - Egypt 4–0 Ethiopia

Mwaka 1959: Egypt
Fainali - Egypt 2–1 Sudan

Mwaka 1962: Ethiopia
Fainali -Ethiopia 4–2 Egypt

Mwaka 1963: Ghana
Fainali- Ghana 3–0 Sudan

Mwaka 1965: Ghana
Fainali- Ghana 3–2 Tunisia

Mwaka 1968:Congo DR
Fainali -Congo DR 1–0 Ghana

Mwaka 1970: Sudan
Fainali - Sudan 3–2 Ghana

Mwaka 1972: Congo
Fainali -Congo 3–2 Mali

Mwaka 1974:Zaire
Fainali - Zaire 2–0 Zambia

Mwaka 1976: Morocco
Fainali -Morocco - guinea

Mwaka 1978: Ghana
Fainali -Ghana 2–0 Uganda

Mwaka 1980: Nigeria
Fainali - Nigeria 3–0 Algeria

Mwaka 1982:Ghana
Fainali - Ghana 1–1 Libya (7–6) penati

Mwaka 1984:Cameroon
Fainali - Cameroon 3 – 1 Nigeria

Mwaka 1986: Egypt
Fainali - Egypt 0–0 Cameroon (5–4) penati

Mwaka 1988: Cameroon
Fainali - Cameroon 1–0 Nigeria

Mwaka 1990: Algeria
Fainali - Algeria 1–0 Nigeria

Mwaka 1992: Ivory Coast
Ivory coast 0–0 Ghana (11–10) penati

Mwaka 1994:Nigeria
Fainali - Nigeria 2–1 Zambia

Mwaka 1996: South africa
Fainali - South Africa 2–0 Tunisia

Mwaka 1998: Egypt
Fainali - Egypt 2–0 South Africa

Mwaka 2000: Cameroon
Fainali - Cameroon 2–2 Nigeria (4–3) penati

Mwaka 2002: Cameroon
Fainali - Cameroon 0–0 Senegal (3-2) penati

Mwaka 2004: Tunisia
Fainali - Tunisia 2–1 Morocco

Mwaka 2006:Egypt
Fainali -Egypt 0–0 Ivory Coast (4–2) penati

Mwaka 2008:Egypt
Fainali - Egypt 1–0 Cameroon

Mwaka 2010:
Fainali- Egypt 1–0 Ghana

Mwaka 2012: Zambia
Fainali - Zambia 0-0 Ivory Coast (8-7) penati

Mwaka 2013:Nigeria
Fainali - Nigeria 1-0 Burkina Faso

Mwaka 2015: Ivory Coast
Fainali- vory Coast 0-0 Ghana (9-8 ) penati

Mwaka 2017:Cameroon
Fainali- Cameroon 2-1 Egypt

Mwaka 2019: Algeria
Fainali -Algeria 1-0 Senegal

Mwaka 2021: Senegal
Fainali - Senegal 0-0 Egypt (4-2 ) penati

Swali ni je nani atachukua kombe hili mwaka huu?

# Hatimaye Tshabalala wakutana

IVORY COAST

BEKI wa kushoto Mohamed Hussein almaarufu Zimbwe Junior au Tshabalala, amekutana na wa jina lake raia wa Afrika Kusini, Siphiwe Tshabalala.

Zimbwe Jr, amenukuliwa akisema katika ukurasa wake wa instagram 'finally', leo nimekutana na role model wangu, mtu ambaye alifanya nizidi kuupenda mchezo wa mpira wa miguu. Alifanya niandike jina lake kwenye jezi yangu."





Kona ya **Urembo**

Na Hidaya Machuppa
Simu: +255 765 828 219

# Ni vipi tunapaswa kuvaa mchuchumio

SERA ya kisigino cha juu ni kanuni au sheria kuhusu kuvaa visigino vya juu, ambavyo vinaweza kuhitajika au kupigwa marufuku katika maeneo na hali tofauti. Visigino virefu vimewekewa vikwazo na sheria na sera katika maeneo mbalimbali kama vile shule, sehemu za hifadhi au makumbusho na maeneo mengine.

Baadhi ya kanuni za mavazi, hata hivyo, zinahitaji wanawake kuvaa visigino virefu ili waonekane kuwa warefu na wa kuvutia zaidi. Viatu hivyo vinaweza kuwa chungu na kuharibu miguu, na kumekuwa na maandamano ya mara kwa mara ya wafanyakazi wanawake dhidi ya sera hizo.





### VITU VYA KUZINGATIA KATIKA UVAAJI WA VIATU VIREFU.

Visigino vya juu vinakulazimisha kutembea kwa urefu na kufanya mavazi ya mtu zaidi. Hata hivyo, kuna baadhi wanafikiri unapaswa kuzingatia.

Kuna maoni mengi juu ya visigino vya juu. Tunaweka pamoja vidokezo na sheria za jinsi ya kupata zile zinazofaa zaidi kwa miguu yako na hafla.

Wanawake wengi hawawezi kutembea kwa visigino vya urefu wa zaidi ya sentimita 10 wakati wote.

Ndio maana tunaishia hapo.

### ANGALIA UMBO LA MGUU YAKO

Viatu vyote vinapaswa kuwa vizuri lakini kwa visigino vya juu ni muhimu zaidi. Viatu vyako lazima visiwe vifupi sana, vyakubana sana au vikubwa sana. Wakati mwingine unaweza kuona «nafasi mashimo» kati ya kisigino na vidole kwa sababu kiatu ni kifupi sana au tight sana. Hii inaweka shinikizo kubwa sana kwenye vidole vyako, ambayo husababisha maumivu na kuharibu miguu yako. Mbali na hilo, inaonekana kutisha.

### USIJARIBU KUNUNUA NAFUU

Kuna sababu mbili kwa nini viatu vya bei nafuu (na wakati mwingine hata ghali) havifurahishi: Visigino ni kabla ya kutengenezwa katika viwanda maalum. Nzuri ni ghali; hata kwa watengeneza viatu.Kisigino lazima iwe katika pembe sahihi kwa kiatu yenyewe. Sio kisigino chochote kinaweza kuunganishwa na mwisho wowote.

### UNATAKA KUVAA JOZI MOJA YA VIATU SIKU ZOTE, HAKI?

Hili linawezekana. Hata hivyo, ni muhimu kujua kwamba visigino vya juu sio stilettos. Ikiwa unakwenda kwa kisigino cha kuzuia, unaweza kutembea bila kujiweka katika hatari.

### NUNUA UREFU UNAOJISIKIA RAHA NAO



Ikiwa tayari wewe ni mrefu unaweza kuwa na furaha na kisigino kidogo. Chochote urefu wako ni, usinunue kitu chochote ambacho tayari unahisi wasiwasi katika duka. Lazima uweze kutembea juu na chini ya duka kwa urahisi. Baada ya yote, urefu wa kisigino haufafanui kiwango cha anasa ya uzuri.

Mtindo na ubora fanya machaguzi sahihi.

### TAFUTA NYENZO SAHIHI ZA VIATU

Visigino ni rahisi sana kuharibika kwa vile uwezekano wa kukwama mahali fulani, mpasuko wa mpira wa kisigino hauna mwisho. Visigino vyema tu ni visigino vya kifahari.

### SAHAU KUHUSU MLIMA EVEREST

Ndio, kuna wakati ambapo haupaswi hata kufikiria kuvaa visigino. Kuna sehemu zingine unaweza kuona wanawake waliovalia visigino virefu wakipanda treni ambayo itawapeleka juu ya mlima. Usiinakili hii.

Milele.Baa kiatu kuangalia na mazingira unayoenda kea usalama zaidi.



> Viatu vyote vinapaswa kuwa vizuri lakini kwa visigino vya juu ni muhimu zaidi. Viatu vyako lazima visiwe vifupi sana, vyakubana sana au vikubwa sana. Wakati mwingine unaweza kuona «nafasi mashimo» kati ya kisigino na vidole kwa sababu kiatu ni kifupi sana au tight sana. Hii inaweka shinikizo kubwa sana kwenye vidole vyako, ambayo husababisha maumivu na kuharibu miguu yako.





Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Januari 24 - 30, 2024 |

# Ivory Coast wapopoa mawe



**Na Mwandishi Wetu**

KITENDO cha Ivory Coast kushindwa kufuzu moja kwa moja katika hatua ya 16 bora ya michuano ya AFCON kimewakasirisha mashabiki wao na kuwafanya waingie mtaani.

Mashabiki hao walifanya vurugu na kupiga mawe magari na majengo kadhaa.

Ivory Coast ambayo ndio wenyeji wa michuano ya AFCON walikubali kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Equatorial Guinea.

Katika Mechi hiyo Ivory Coast walipachika mabao mawili lakini yalikataliwa kwa kuwa wafungaji walikuwa wameotea.

Wachezaji wa timu hiyo alilazimika kuondolewa na polisi kwenda vyumba vya kubadilishia nguo.

Sasa wenyeji wanasubiri kudra ya Best looser ambayo itachukua timu nne.

Vigogo wengine Ghana nao wameaga mashindano hayo huku Nigeria wakifanikiwa kusong a mbele sawa na Guinea, Misri

# Stars kuandika wasifu mpya?



**Na Mwandishi Wetu**

SUALA si kushiriki michuano ya soka ya Mataifa ya Afrika bali janbo la msingi ni kuingia hatua ya 16 bora.

Taifa Stars watoto wa Mama Samia Suluhu, leo wanashuka kupambana na Congo DR katika mechi ambayo inaenda kuandika historia.

Ni wazi Stars hawataki kuandika wasifu mfupi kwamba walikwenda AFCON wakacheza mechi tatu wakatolewa.

Mabadiliko katika benchi la ufundi yameonekana kurudiaha morali ya wachezaji.

Makocha Hemed Morocco na Juma Mgunda wanataka kuthibitisha kuwa hata makocha wazawa wakiaminiwa wanaweza.

Stars inahitaji kushinda mechi ya leo itakayofanyika saa mbili usiku.

Ikiwa na pointi moja ikishinda itafikisha pointi nne huku Congo wakibaki na pointi mbili na ikiombea sare katika mechi kati ya vinara Morocco wenye pointi nne na Zambia wenye pointi mbili.

Ushindi wa Zambia utavuruga nafasi ya moja kwa moja ya Stars kusonga mbele labda wawe wameifunga Congo kwa zaidi ya mabao matatu. Kwa kuwa tayari Morocco wana zaidi ya mabao manne.






## Ratiba ya leo

| | |
|---|---|
| Namibia Vs Mali | 02:00 Usiku |
| South Africa Vs Tunisia | 02:00 Usiku |
| Tanzania Vs DR Congo | 05:00 Usiku |
| Zambia Vs Morocco | 05:00 Usiku |

## Mataifa yaliyofuzu hatua ya 16 BORA ya AFCON mpaka sasa.

1. Angola
2. Burkina Faso
3. Cape Verde
4. Misri
5. Equatorial Guinea
6. Mali
7. Nigeria
8. Senegal
9. Afrika Kusini

# Shabiki afungiwa kwa ubaguzi

**MILAN, Italia**

SHABIKI mmoja wa Soka amefungiwa miaka mitano kuingia kwenye viwanja vya Soka kutokana na vitendo vya kibaguzi dhidi ya kipa Mike Peterson Maignan wa AC Milan

Aidha, jimbo la Udine limemfungia maisha mtu huyo kwenye uwanja wao wa Bluenergy.

Maignan alionekana akibishana jambo na refa kabla ya kuvua gloves zake na kuondoka uwanjani huku wachezaji wenzake wakiwafuata.

Tukio hilo lilisababisha mechi kusimamishwa kwa takribani dakika 10.

Akizungumza na mtandao mmoja wa nchini Italia, Maignan ambaye pia ni mchezaji wa timu ya taifa ya Ufaransa amesema " walikuwa wakizomea na kusema nyani na hii si mara ya kwanza kwangu"

"Wakati mechi ikianza walikuwa wakipayuka hivyo hivyo, nilimuarifu refa na tangazo la wazi lilitolewa kuwataka mashabiki waache mara moja kitendo hiko".

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Italia Matteo Piantedosi amelielezea tukio hilo kuwa ni la kuchukiza.

Polisi wanachunguza tukio hilo kupitia Camera za CCTV na mitandao ya kijamii ili kujaribu kuwatambua watu wengine ambao huenda walihusika katika tukio hilo.

